ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole

35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani

49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 3 April, 2010

(Mkutano ulianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*P.A.C*) 2009/2010

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Mspika, awali ya yote naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliya afya na uwezo kwa siku ya leo kuweza kuendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya kamati yangu katika Baraza lako hili tukufu. Napenda kwa aina ya pekee kutoa shukurani zetu za dhati kabisa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kutokana na mashirikiano makubwa waliyoyaonesha wakati wote wa kazi za kamati.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali kwa mashirikiano ya pamoja waliyoyaonesha ndani ya kamati pamoja na jitihada yao ya kufanya kazi kwa bidii bila ya kuchoka.

Mhe. Spika, naomba kwa nafasi ya kipekee kabisa sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati hii ambao kwa mashirikianao yao makubwa wameiwezesha kamati yake vizuri na kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni kama wafuatao:-

1.	Mhe.	Fatma Abdulhabib Fereji	Mwenyekiti
2.	Mhe.	Omar Ali Shehe	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe.	Abbass Juma Muhunzi	Mjumbe
4.	Mhe.	Ali Mohamed Bakari `	Mjumbe
5.	Mhe.	Anaclet Thobias Makungila	Mjumbe
6.	Mhe.	Hija Hassan Hija	Mjumbe
7.	Mhe.	Nassor Ahmed Mazrui	Mjumbe
8.	Mhe.	Mkongwe Nassor Juma	Mjumbe
9.	Mhe.	Said Ali Mbarouk	Mjumbe
10.	Mhe.	Thuwaybah Edington Kisasi	Mjumbe
11.	Ndg.	Shemsa Maabad Mohamed	Katibu
12.	Ndg.	Othman Ali Haji	Katibu

Mhe. Spika, Kamati yetu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika imefanya kazi kwa mujibu wa kanuni ya 113 ya Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2009. Kamati hii imefanya kazi kubwa sana kwa kutumia muda mdogo kulingana na hali halisi ya bajeti ndogo ya Baraza katika kazi za kamati hususan kwa mwaka huu wa fedha 2009/2010.

Hata hivyo, kamati imeshindwa kufuatilia Ripoti nzima ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka huo tuliokuwa tukiufanyia kazi wa 2007/2008. Hivyo, inategemea kumaliza kazi hiyo katika kipindi kijacho cha kazi za kamati.

Mhe. Spika, naomba ieleweke kwamba, ripoti ninayowasilisha hapa ni muhtasari wa ripoti kamili ya *P.A.C* iliyopo kwenye ukurasa kuanzia wa 85 hadi 110 wa kitabu cha Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, kutokana na majukumu mazito waliyopewa Kamati ya *P.A.C* ya kufuatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo inajumuisha katika ukaguzi wake Wizara zote za Serikali, Idara, Mashirika na Halmashauri zote, kamati inashauri iongezewe muda wa kufanya kazi ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA

Mhe. Spika, kuhusiana na uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Kutokana na Sheria ya Fedha Nam 8 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2), kinaeleza wazi wajibu wa Taasisi za Serikali kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha (kwa hiyo, uwasilishaji usizidi tarehe 30/9 ya kila mwaka).

Kamati imethibitisha kwamba, kati ya taasisi 31 ni taasisi 6 tu zimeweza kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka (2007/2008) kwa wakati. Hali hii huathiri utekelezaji mzima wa majukumu ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hupelekea kutofanyika kwa kazi ya ukaguzi kwa ufanisi. Hivyo, kamati inashauri kuchukuliwa hatua za kiuwajibikaji kwa idara na taasisi zote zinazochelewesha na zinazoshindwa kuwasilisha kabisa hesabu zao za mwisho wa mwaka.

DAFTARI LA KUDUMU LA KUHIFADHIA MALI ZA SERIKALI (*Fixed Assets Register*)

Mhe. Spika, kamati imeendelea kusikitishwa na taarifa ya kukosekana kwa daftari la kuhifadhia mali za kudumu kwa takriban katika Taasisi zote za Serikali. Taarifa iliyokuwa ikitolewa mbele ya kamati kuhusiana na hoja hii ni kuwa unasubiriwa muongozo kutoka Wizara ya Fedha chini Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma. Kamati inasisitiza ni wajibu wa kila Afisa Muajibikaji (*Accounting Officer*) wa taasisi kuharakisha kukamilisha muongozo huo na kujiandalia utaratibu wa kuzitambua na kuzirekodi mali zao zote wanazozimiliki katika madaftari maalumu wakati wanasubiri muongozo kutoka Wizara ya Fedha. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa taasisi nyingi hazina hata kumbukumbu za mali za umma wanazozimiliki na pahala zilipo.

Sambamba na hili, Taasisi nyingi za Serikali zinamiliki majengo bila ya kuwa na uthibitisho wa kisheria wa umiliki wa majengo hayo. Hii inakuwa ni sawa na kuwa na hifadhi (*Possess*) lakini hazina umiliki (*ownership*) wa mali hizo. Tatizo hili halipo kisheria tu, lakini pia serikali inakosa kujua *"Countries Capital Worthness"* kwa kujua idadi na thamani ya mali zake inazozimiliki.

Kamati inaishauri serikali kuchukua jitihada za makusudi kurekebisha mapungufu haya makubwa ambayo yanaisababishia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kutoa picha halisi ya Hesabu za serikali.

MADENI SUGU

Mhe. Spika, ukaguzi wa kamati umebaini kuwa katika taasisi mbali mbali za serikali kuna madeni sugu na ya muda mrefu. Katika jitihada za kulitatua tatizo hili, Kamati ya *PAC* iliandaa kikao rasmi cha kuwakutanisha wizara, idara na taasisi zote zenye madeni sugu. Mhe. Spika, kamati imefikia muafaka kuwa suala hili lishughulikiwe baina ya Afisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kutafuta utaratibu wa kisheria wa kuyashughulikia madeni hayo.

UPOTEVU WA MISHAHARA

Mhe. Spika, kamati imeshtushwa na taarifa za upotevu wa mishahara katika taasisi mbili. Kwa upande wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, jumla ya shilingi 23,240,556 zimepotea na kuisababishia hasara kubwa serikali. Aidha, shilingi 4.8 zimeripotiwa kupotea katika Wizara ya Afya, Pemba. Kamati imeripotiwa kuwa kesi hizo zipo Mahakamani, lakini inasikitishwa na taarifa kwamba, haki za wafanyakazi hao walioibiwa mishahara yao hadi sasa bado hawajalipwa. Kamati inaagiza wizara zinazohusika kuwalipa wafanyakazi hao haki zao. Aidha, kamati iarifiwe juu ya matokeo na maendeleo ya kesi hizo zilizoko mahakamani na hatua zilizochukuliwa kwa wale waliobainika kutenda makosa hayo.

UVAMIZI WA SHAMBA LA MAKURUNGE

Mhe. Spika, kama ilivyoripotiwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hoja nambari 33.1 inayohusu uvamizi wa mashamba ya serikali. Kamati imesikitishwa sana kwa kuzipoteza mali nyingi za serikali zilizokuwepo Makurunge zikiwemo nyumba, skuli, shamba lenyewe pamoja na raslimali watu. Uvamizi huo umesababishwa zaidi na kutokupewa kipaumbele kwa shamba hilo ambapo hapo awali lilikuwa ni tegemeo kubwa kwa serikali na ni kitega uchumi muhimu, pia kukosekana kwa hati miliki ya shamba hilo kumechangia kukwamisha kufanyika kwa maendeleo muhimu ya kuliendeleza shamba hilo. Baya zaidi ni kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano imeshalichukua shamba hilo la Makurunge na kuibakishia Zanzibar asilimia 20 tu ya eneo lililokuwa likimilikiwa kabla.

Mhe. Spika**,** kamati imepata muda wa kulitembelea shamba hilo na kuonana na uongozi wa Wilaya ya Bagamoyo akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo pamoja na jopo zima la watendaji wake katika wilaya hiyo kwa lengo la kutafuta muafaka wa upatikanaji wa hati miliki ya Shamba la Makurunge ambapo serikali ilipewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano tangu mwaka 1969.

Mhe. Spika, kikwazo kikubwa kilichokuwa kinakwamisha upatikanaji wa hati miliki ya shamba hilo ilikuwa ni pamoja na shamba hilo kumilikiwa na serikali. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kwamba umiliki wa shamba hilo sasa utakuwa chini ya Chuo cha Kilimo, Kizimbani.

Mhe. Spika, kamati inasisitiza sana kuharakisha taratibu za kutafutwa kwa hati miliki ya shamba hilo ikiwa ni pamoja na kuandaa mchakato mzima wa matumizi yake na kuwasilisha katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ili uweze kufanyiwa kazi na hatimae kupatiwa hati miliki. Aidha, kamati inashauri

kwa vile shamba hilo litakuwa linamilikiwa na Chuo cha Kilimo cha Kizimbani, chuo ambacho kimejikita na kufanya utafiti katika mambo yanayohusiana na kilimo tu, juhudi za makusudi zifanyike za kuongeza wigo zaidi wa utafiti ambao utaingiza mambo ya utalii, viwanda vidogo vidogo vya kuzalisha chumvi na mazao mengine ya baharini ili waweze kulitumia shamba hilo kwa ufanisi.

UPOTEVU WA MALI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, kamati imefadhaishwa na hoja ya wizi wa kompyuta uliotokea katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na zaidi baada ya kuhoji, imefahamika wazi kwamba, juhudi za makusudi za hatua za kufuatilia wizi huo na hatimaye kuwawajibisha wahusika kisheria, hazijachukuliwa ipasavyo. Kamati imefahamishwa kwamba, afisi baada ya kutokea wizi huo ilitoa taarifa Polisi. Hadi Kamati ilipofika kwa ukaguzi hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kukabiliana na wizi huo. Hivyo, kamati inashauri ikithibitika kuwa ni upotevu, afisi ipeleke ripoti ya maandishi juu suali hili katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kama ni upotevu kwa hatua za utekelezaji, kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 22 cha Kanuni za Fedha mwaka 2005.

MAPUNGUFU KATIKA SHUGHULI ZA MANUNUZI

Mhe. Spika, kamati ilifuatilia kwa karibu hoja namba 57.6 ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2007/2008 ambayo inahusu Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Hoja hii inahusu ununuzi wa samani (*furnitures*) kwa ajili ya Afisi ya Wilaya ndogo ya Kojani, Pemba ambapo shilingi 71,620,000/- milioni zilitumika wakati kumeripotiwa kuwepo kwa upungufu wa samani zenye thamani ya shilingi 21,380,000/- milioni zilizokuwa tayari zimeshalipiwa lakini hazikuonekana katika Afisi ya Wilaya Ndogo ya Kojani pamoja na kugundulika kuwa viwango vya bei vilivyotumika kwa ununuzi wa samani hizo ni vya juu sana kulinganisha na samani zenyewe halisi zilizoonekana katika ukaguzi.

Mhe. Spika, kamati inaishauri Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kufuatilia kwa umakini zaidi shughuli zinazofanywa na watendaji kuhusiana na manunuzi na kuhakikisha zinafanyika kwa kuzingatia sheria ya fedha na ya manunuzi za mwaka 2005. Pia kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inapatikana kwa vifaa vilivyonunuliwa.

UWASILISHAJI WA MAPATO YA SERIKALI

Mhe. Spika, kamati imegundua kuwa kuna tabia ya baadhi ya Taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kujikopesha mapato hayo kwa matumizi ya afisi zao kabla ya kuyawasilisha benki kwa wakati. Tatizo hili limeonekana katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale. Kutowasilisha fedha benki kwa wakati ni kwenda kinyume na kifungu cha 77(1) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005. Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za kisheria kwa wale wote watakaoendelea na tabia ya kujikoposha fedha za mapato wanayoyakusanya kabla ya kuziwasilisha benki.

UENDESHAJI WA HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Spika, kamati imegundua kuwa kuna baadhi ya taasisi hazijiendeshi vizuri kutokana na kukosekana kwa bodi zenye uwezo wa kutoa maamuzi ya namna ya uendeshaji wa taasisi hizo. Hili limedhihirika katika Hoteli ya Bwawani kwamba pamoja na kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza, uongozi wa Hoteli unashindwa kuiendeleza hoteli ipasavyo kutokana na kukosa chombo chenye uwezo wa kushauri ipasavyo na kutoa maamuzi ya haraka na ya ufanisi. Hivyo, kamati inashauri kwamba, Taasisi za Serikali zinazojitegemea na zenye muundo wa kibiashara mfano mzuri ikiwa ni Hoteli ya Bwawani kutumika utaratibu wa kuwa na bodi zao wenyewe zenye mamalaka ya kutoa maamuzi ya kujiendesha kibiashara.

UDHIBITI WA NDANI *(Internal Controls)*

Mhe. Spika, vile vile kamati imegundua kwamba, kukosekana kwa udhibiti wa ndani na kukosekana kwa Mkaguzi wa Ndani ambaye ataweza kuangalia mwenendo mzima wa matumizi ya taasisi husika ni tatizo kubwa linalopelekea upotevu wa fedha za serikali. Kwa mfano, matatizo haya yamebainika katika Hoteli ya Bwawani ambapo katika mwaka wa fedha 2007/ 2008 wameshindwa kutayarisha ripoti ya fedha ya mwisho wa mwaka, ripoti hiyo husaidia kutoa picha halisi ya mahesabu ya hoteli kwa serikali.

Kwa upande wa Shirika la Huduma za Maktaba ukosefu wa udhibiti wa ndani umepelekea upotevu wa Tsh. 26,963,500/-. Hali ya kutokuwepo Mkaguzi wa ndani imempa fursa mhasibu wa Shirika la Huduma za Maktaba kufanya maamuzi yake pekee na kufanikisha kuondoka na fedha nyingi za walipa kodi. Kamati inashauri kuona umuhimu wa kuwekwa wakaguzi hao kila panapohitajika ili kunusuru upotevu wa fedha na kutoa ushauri kwa uongozi.

CHANGAMOTO

Mhe. Spika, kamati yetu inakabiliwa na changamoto nyingi sana katika utekelezaji wa majukumu yake. Miongoni mwa changamoto hizo ni suala la muda. Kamati yetu na zaidi kwa mwaka huu wa fedha, imepata muda mdogo sana wa kufanya kazi kwani ilipata karibu wiki 6 tu, ukilinganisha na Kamati nyengine za Kudumu za Baraza. Kwa kuzingatia hoja hii, kamati yetu haikuweza kufanya kazi kwa ufanisi na matokeo yake kuna kazi nyingi zimebakia.

Mhe. Spika, ili kukabiliana na kasoro hiyo iliyojitokeza, Kamati yetu inapendekeza iongezewe muda ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa wakati uliopangwa. Mfano mzuri ni wa kitabu hichi cha mwaka 2008/2009 hadi leo tunawasilisha ripoti hii katika Baraza lako bado tuna kazi ya ripoti hiyo haijamalizika, ukizingatia kuwa ni vyema kuwasilisha ripoti yetu ikiwa imekamilika. Hivyo, tunashauri kuzingatiwa kwa ombi letu hilo ili tuweze kufanya kazi zetu kwa ukamilifu.

Miongoni mwa changamoto nyengine zinazoikabili kamati yetu ni pamoja na haja ya kuongeza uelewa kwa Waheshimiwa na zaidi unaohusiana na masuala ya fedha ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Masuala ya Fedha yanahitaji uelewa mkubwa na zaidi kwa kuzingatia utekelezaji wa majukumu yetu, siku zote kamati yetu inakabiliwa na kujenga hoja mbele ya watendaji wa wizara na taasisi nyengine ili kuibua ukweli unaohitajika.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Kamati wana kilio cha kutaka kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara yanayohusiana na mambo ya fedha, taratibu za manunuzi na masuala muhimu yanayohusu ukaguzi wa thamani (*value for money audit*). Mhe. Spika, mbali na haja hii, kamati pia inashauri Baraza kuweza kuipatia usafiri wakati wa kazi zake ili kuepusha kuanza kufadhiliwa na wakaguliwa kwani huipunguzia hadhi kamati yetu.

Mhe. Spika, kwa heshimma kubwa naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwa uwasilishaji huo mzuri wa ripoti ya kamati. Ripoti imetaja mengi ambapo wajumbe sasa inabidi tujadili.

Wakati huo huo niwakumbushe Waheshimiwa Mawaziri kwamba baadae tutataka tusikie kauli kutoka kwa wizara mbali mbali kutokana na yale ambayo yametajwa ambayo mengine ni upotevu wa fedha za moja kwa moja, lakini maeneo mengine ni ya masuala ya wakaguzi wa ndani hasa Wizara ya Fedha pamoja na mengine katika wizara mbali mbali kama vile Wizara ya Kilimo,

Mifugo na Mazingira na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na wizara nyenginezo. Sasa basi ripoti hii ijadiliwe.

Lakini kabla ya kujadiliwa ripoti hii, nataka tujikumbushe tu kwama tuna tatizzo la muda, tunazo ripoti mbili ambazo zinataka zijadiliwe, hii na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na shughuli zetu leo tulijipanga zimalizike kipindi hiki cha asubuhi si zaidi ya saa saba kama inavyoelekezwa na kanuni.

Kwa hivyo, tumepanga tutumie si zaidi ya muda wa saa moja na dakika 45 kwa kamati hii ambayo ripoti yake imeshawasilishwa. Na saa moja na nusu kwa ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na baadae tumuachie Mhe. Waziri Kiongozi kama dakika 45 ili nay eye kuwasilisha taarifa ya kufunga mkutano leo.

Hii inatokana na kwamba leo ni siku maalum tuliiongeza kwa mara ya kwanza na kushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kukubali kufanya kazi siku ya leo ya Jumamosi wakati tuko katika shamra shamra ya sherehe za Ijumaa Kuu na Pasaka kwa pamoja, hasa hasa kwa upande wetu tunao wageni wetu wa kawaida wapo hapa toka jana mnamo saa tisa jioni. Nalo ni jambo muhimu sana ambalo kwa kawaida tuna mashirikiano na mahusiano ya muda mrefu ambayo tunapenda tuyadumishe. Sasa jioni tutakuwa na mambo mengine pamoja na wageni wetu hao ambayo nayo ni ratiba maalum inayotuhusu sisi Waheshimiwa Wajumbe.

Kwa hivyo, tujaribu kujibana kwa muda katika kuchangia, lakini itapofika wakati sasa nitakuwa nawaita mawaziri na baadae mwenyekiti ili kumaliza shughuli ya kamati hiyo. Tuanze basi kumsikiliza Mhe. Haji Mkema Haji, jitahidi utumie dakika kumi.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuniteuwa kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa ripoti ya Kamati ya *PAC.*

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mwenyekiti namna alivyowasilisha ripoti yake kiufundi, lakini nimpongeze yeye pamoja na kamati nzima kwa kazi zao walizozifanya na kutizama hesabu za serikali juu ya matumizi yetu na kutuletea ripoti kamili ambayo itatupa mwanga na sisi kuweza kuchangia matumizi ya serikali kama ilivyo kwenye kitabu.

Mhe. Spika, mimi ninahusika na ukurasa wa 85 kifungu 1.4 cha ripoti ya Kamati na pale ambapo panaelezea matumizi mabaya. Zimetajwa taasisi tatu pale. Kwanza Kikosi cha Valantia jumla ya shilingi 12,733,450/-. Hizi wenzetu mpaka wameripoti pale bado hazijulikani matumizi yake wala stakabadhi.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii jumla ya shilingi 61, 187,500/-, lakini pia Shirika letu la Utalii US$ 12,545.
Mhe. Spika, kwa kweli hili linasikitisha, nchi yetu ilivyokuwa changa, bajeti yetu finyu, lakini tunapewa fedha hizi katika maidara yetu na matumizi yake yanakwenda ovyo, hili si la kuachiwa.

Wakati huo huo wananchi wetu wanapiga kelele huduma haziendelei hasa kama hii Wizara ya Afya, shilingi 61.187.500/- si pesa kidogo unaweza kupata magodoro ya hospitali nzima wakaweza kulalia wagonjwa, lakini hapa zimetumika hazijulikani. Shirika la Utalii linasuasua lakini bado wametumia pesa ovyo dola 12 elfu, kwa kweli inasikitisha.

Nakuja kwenye ukurasa wa 86, hapa pana madeni lakini mimi nitazungumzia kuhusu madeni ya wawekezaji kwenye kodi ya ardhi. Mhe. Spika, vyanzo vyetu vya mapato ni kidogo, raslimali hatuna, zile raslimali chache tulizonazo basi ndizo tunazozitegemea katika kupata mapato. Nastaajabu na kwa nini wenzetu tumewapa madaraka juu ya huu ukusanyaji hasa kwa wawekezaji. Kwa sababu wawekezaji wao wanakuja kutafuta pesa kwetu, wanapata na sifikirii kama wanakula hasara kwa sababu wangekuwa wameshahama, lakini kulipa kodi hawataki sijui kwa nini.

Mimi hapa nina wasi wasi, pengine hao wamefanya kiburi kwa makusudi labda na sisi tunakwenda kinyume, tunapata chochote tunawastahamilia. Huo ndio wasi wasi wangu mimi kwa sababu mwekezaji mgeni afanye kiburi asitake kulipa kodi haijatokezea nchi yoyote, kodi ya serikali inalipwa ipasavyo.

Mwaka jana ilijitokeza hivi hivi Mhe. Spika, tukasema kama imekuwa hivyo basi tuwazuilie leseni wasifanye biashara si wanapata hasara hawawezi kulipa kodi, kwa nini waendelee. Lakini bado katika ripoti hii wenzetu wameona bado wawekezaji wanaopewa ardhi kwa kuwekeza hawataki kulipa kodi.

Mhe. Spika, mimi hili sikubaliani nalo kabisa kuwa liendelee, serikali lazima iwe kali na ihakikishe fedha hizi tunapewa ripoti yake katika bajeti kuwa zimesharejeshwa serikalini. La si hivyo hii Idara ya Ardhi Mhe. Spika, pengine mimi nitakuwa mgumu, wenzangu waliahidi watazuia shilingi na mimi nitazuia fungu kwenye idara hii. Kwa nini wanashindwa kukusanya fedha kwa wawekezaji. Maana wananchi walitaka viwanja hapa hawakupata lakini wawekezaji wameshapewa huko maeka kwa maeka na hawalipi kwa nini na hapa si kwao. Mhe. Spika, hilo mimi nasema tulitie mkazo hasa kwa wenzetu wa ripoti hii.

Mhe. Spika, nimalizie katika ya jumla jumla amezungumza Mhe. Mwenyekiti juu ya upotevu wa mishahara. Hii imekuwa kilema katika serikali yetu kusikia

leo hapa pamevunjwa inakuwaje. Mambo haya kipindi kirefu yalikuwa hayajatokezea kuna kasoro gani. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha aje atujibu, miaka yote mimi sijasikia mambo haya ya kuwa mishahara imeibiwa. Lakini hata kwenye vikosi kwa nini na linaendelea. Kama imetokezea mara moja lakini leo kikosi hichi, unakwenda kama moto ulioingia kwenye nyika. Wizi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, leo mara Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na mwengine mna rejea kwa rejea.

Mhe. Spika, hili limekuwa donda ndugu na lazima Mhe. Waziri wa Fedha atwambie inakuwaje. Hao wahasibu hawafanyiwi *vetting*, tunacho kitengo chetu, basi kama hawawezi kuwafanyia hivyo bora tukivunje. Mhe. Spika, watu wanaoshughulika na fedha lazima tuwatazame kweli wanafaa waaminifu tuwakabidhi. Tumeweka kitengo maalum kabla hatujawaajiri wanafanyiwa vetting hao, kwa nini basi wanabakia watu wasio waaminifu wanapoteza pesa za umma, pesa za wananchi wanyonge. Mhe. Spika, naomba na hili litazamwe.

Mhe. Spika, mwisho hawa wenzetu wamefanya kazi nzuri hasa wanapobaini upotevu wanakwenda chini kabisa, sisi kamati nyengine tunakwenda juu juu. Lakini Mhe. Spika, ningekuomba nitumie nafasi hii kamati hii ukaipa siku angalau tano za ziada, kuna kazi muhimu sisi wenzao tumeacha kiporo jinsi matumizi ya ujenzi wa Afisi ndogo Kojani. Hii Mhe. Spika, naiomba maalum ikatazame, kazi haikuturidhisha, vifaa vilivyonunuliwa kweli havituridhishi, watutengenezee ripoti kikao kijacho watupe na sisi tuweze kutoa kauli juu ya kitendo kile.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nakuomba uwapatie siku hizi kwa sababu sisi hatukuweza kwenda mpaka kwenye vitabu kwa mujibu wa utaratibu wetu. Hawa wenzetu wana nafasi ya kwenda *deep*. Mhe. Spika, baada ya kumaliza ombi langu nakushukuru sana.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuzungumza machache tu katika mchango wangu ambao nitawasilisha sasa hivi.

Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba niungane na wenzangu sisemi kamati yangu iongezewe muda wala kamati nyengine yoyote iongezewe muda, nasema kwamba tubadilisheni kanuni kwa sababu ya muda unaopewa kamati zote hautoshi. Kila atakayekuja hapa atajipigia debe mwenyewe kamati, lakini ukweli ni kwamba muda tunaopewa kufanya kazi za kamati hautoshi. Sasa kwa kuwa tunakwenda kwa mujibu wa kanuni basi tuone kwamba katika kipindi kijacho tunabadilisha kanuni kuongeza muda. Tunapoongeza muda maana yake kwamba tuwaambie na hao wanaotuletea pesa hizi basi watengeneze na maposho ili tuweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, mimi nina moja na nitalenga kwa upande wa Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani sina kumbukumbu nzuri imeanzishwa lini lakini nafikiri kwenye miaka ya 90. Mhe. Spika, nadhani tokea ilipoanzishwa hoteli hii sijui kama tumepata mafanikio yoyote. Sasa hivi inatisha, imefikia wakati kuona kwamba hoteli hii kwa sababu ya uendeshaji wake pengine si mzuri sana na ndio maana tunaingia katika matatizo, pengine hakuna bodi zinazoongoza.

Mhe. Spika, juzi nimemsikia Mhe. Waziri hapa ameulizwa swali hilo linalohusu habari ya bodi, lakini bodi hizi bado hazijaundwa. Pia alizungumzia masuala ya kukaimu na akatuhakikishia kwamba katika kipindi kijacho hakutakuwa na kaimu tena.

Mhe. Spika, nimesikia katika vyombo vya habari kwamba hoteli hii iko katika soko la mnada na hii ni hoteli ya serikali. Je, Mhe. Waziri hivi hizi kauli tunazozisikia zina uhakika ni sahihi. Kama hoteli hii itauzwa tutakuwa na nini cha kujivunia. Lakini pili iwapo itauzwa hoteli hii kwa nini ifikie taasisi kubwa kama hii ya serikali iuzwe kwa ajili ya madeni.

Sasa Mhe. Spika, hili mimi nilisema niliulize makusudi tupate uthibitisho wa uhakika wa serikali kuona kwamba kweli hoteli yake inauzwa. Kwa sababu hizi tetesi au sijui sahihi mara nyingi tunasoma kwenye magazeti na tunasikia kwenye redio. Lakini nadhani kwa sababu waandishi wengine baadhi yao wanakuwa wako sahihi, baadhi ya waandishi wengine wanakuwa wachafuzi. Wanatafuta jambo moja dogo tu watalikuza liwe kubwa na hasa jambo likiwa linagusa gusa mambo ambayo hayaendani vizuri basi wanalikuza linakuwa kubwa.

Mhe. Spika, hizi kauli za waandishi walizozitoa zina uhakika, hoteli hii kweli iko katika mnada wa soko. Mhe. Spika, nilikuwa na hayo tu, ahsante.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: *Bismillahi Rahmani Rahiym.* Mhe. Spika, ahsante sana kunipa fursa hii ya kuchangia na mimi katika ripoti hii ya Kamai ya *PAC*. Mimi ni mmoja katika wajumbe wa kamati hii na nahisi kwamba yako mengine naweza kujaliza au kuyatilia mkazo katika yale yaliyozungumzwa hii leo.

Mhe. Spika, kwanza suala la hili buku la kuhifadhia mali la serikali.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, Makatibu Wakuu wa Wizara zetu na Katibu Mkuu wa Wizara yangu ya Afya na Ustawi wa Jamii

amenipigia simu kwamba ameambiwa ndani kumejaa na yeye na wenziwe wako juu na nafasi ipo. Ni vizuri waje wasikie nini waheshimiwa wanazungumza. Kwa sababu sasa hivi tunazungumza mambo yanayohusiana na fedha na wao ndio watumizi wakubwa wa fedha.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba wapatiwe hizi nafasi tupu waje wasikie nini michango ya waheshimiwa hapa Barazani.

Mhe. Spika: Tunakushukuru watendaji fanyeni hiyo kazi. Makatibu Wakuu ni vizuri wakawepo hapa wakapata maelezo ya moja kwa moja kwa sababu wao ndio *Accounting Officers* wa wizara zinazohusika. Watendaji fanyeni hiyo kazi.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Spika, tumetembelea katika taasisi nyingi tatizo sugu lililoko ni kwamba suala la muundo wa buku la kuhifadhia mali za serikali bado haujatoka katika Wizara ya Fedha mpaka dakika hii. Mimi naomba kusisitiza kwamba hili ni suala muhimu sana Wizara ya Fedha wasilidharau kwa sababu *worthiness* ya serikali inapatikana kutokana na mali zilizonazo. Kwa bahati mbaya taasisi na wizara nyingi buku hili halipo na hivyo basi hawawezi kujua wana mali kiasi gani, wana hasara kiasi gani na faida kiasi gani. Kwa sababu hata hawajui mali zao walizonazo.

Mhe. Spika, vile vile hawana hati miliki ya majengo ya afisi zao, wala maskuli yao. Ukenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hawajui thamani ya skuli zao walizonazo, majengo yao waliyonayo. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii halikadhalika na mawizara yote. Huu si mwendo mzuri wa kwenda na serikali, lazima kila wizara ijue ina majengo ya thamani ya kiasi gani au mashamba ya kiasi gani, pia wanakuwa na hati miliki ya yale maofisi yao na majengo yao waliyonayo.

Kwa mfano, Kikosi cha Valantia, Kikosi cha Zimamoto wote hawa hawana hati miliki ya majengo yao, wala hawajui majengo yao yanagharimu kiasi gani. Hili si suala la kukaliwa kitako, ni suala la kufanyiwa kazi tuone kwamba serikali inajua ina uwezo wa kiasi gani, *worthiness* ya serikali ni kiasi gani. Hiyo itawapa zaidi msukumo wafadhili na watu mbali mbali ambao watataka kuchangia katika maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati bila ya kusubiri mtiririko uliokuwa unachelewa kwa muda mrefu kutoka Wizara ya Fedha, lakini wameona kwamba hawawezi kufunga mahesabu yao, wala hawawezi kuendesha idara zao bila ya kuwa na mabuku hayo. Mabuku hayo wameyaweka tena yako katika hali nzuri, tena yako katika mtiririko wa kitaalam kabisa.

Naomba niwapongeze kwa dhati Idara ya Maji, *ZSTC* na Shirika la Bandari. Hawa mabuku wametayarisha na wameweka kila kitu chao mpaka ile bandari ya Zanzibar thamani yake ni kiasi gani, mpaka kufikia muda fulani itakuwa thamani yake imeshuka kwa kiasi fulani. Hii ni mifano ya kuigwa na taasisi nyengine zote zile kwa sababu Wizara ya Fedha imeshindwa kuweza kuandaa huo muundo, lakini bado idara hizi zimechukua hatua thabiti kuhusu suala hili. *(Makofi).*

Mhe. Spika, jengine Polisi kwamba hawako *serious* na wizi wa mali za serikali. Kwa sababu mali za serikali zinaibiwa hawana ufuatiliaji wala hakuna ripoti zinazokuja, pale palipoibiwa watu wamenyamaza kimya. Kwa hivyo, mimi naagiza kwamba ipo haja ya polisi kuona kwamba mali za serikali zinachukuliwa hatua zinapoibiwa ili kukomesha wizi kama ule usiendelee.

Mhe. Spika, jengine ambalo tumeliona ni wizi wa mishahara. Mhe. Spika, mishahara inaibiwa na la kusikitisha kwamba mtu mmoja au kikundi cha watu kinashajiisha kuiba mishahara ya taasisi fulani halafu wafanyakazi kama mia na kitu hawana mshahara. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha alisema kwamba sisi bwana hatuwezi kulipa mishahara mpaka kesi imalize Mahakamani.

Mimi nasema kwamba sisi *private sector* ikitokezea wizi wa mishahara basi kama hujawalipa mishahara yao jamaa maandamano tayari, mgomo tayari wanakwenda mbele hali inakuwa si shwari. Serikali inatulazimisha walipeni mishahara kesi ikimalizika mtakuja kulipana wenyewe. Nashangaa upande wa serikali Mhe. Waziri wa Fedha kasema kwamba mpaka kesi imalizike. Hawa wafanyakazi watakula nini, wamekopa, waendelee kukopa kwa sababu hapo wizi unazidi kuendelea.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri alitafakari suala hili waajiri wale wapewe mishahara yao na baadae ikiwa Mahakamani kumetoka hukumu ya kulipwa mishahara ile, basi serikali ibebe jukumu lile la kulipa hicho kidogo kidogo kitakachokuja kwa huyo aliyeiba. Lakini naomba wale waajiriwa wapate mishahara yao angalau wajikomboe, maisha ni magumu, matumizi ni makubwa, mishahara midogo tuwasaidieni jamani.

Mhe. Spika, jengine tulipokwenda katika Kikosi cha JKU tukamkuta Mkuu wa JKU anakaimu kwa muda wa miaka miwili sasa, nahisi kwamba kukaimu kwa muda mrefu kama huo katika kikosi muhimu kama hichi si jambo la busara. Aidha, ningeomba Kaimu Mkuu wa JKU yule madaraka yale apewe awe ndio Mkuu wa JKU au atafutwe anayefaa aweze kuwa Mkuu wa JKU. Lakini kikosi kama kile kuendelea mpaka dakika hii ikawa bado mtu anakaimu tu mpaka lini hili si suala zuri sana.

Mhe. Spika, jengine tumekwenda kwa Mrajis wa Serikali, huyu ndie tunayemtegemea yeye anarajis makampuni yote, mikataba yote na mambo mengine yote, huyu Mrajis mpaka leo gari hana anakwenda kwa miguu ni heshima gani. Yule mtu anayekwenda kule ku-*register* kampuni yake akimuona huyo Mrajis wenyewe anakwenda kwa miguu gari hana au gari kweche kweche atakuwa na imani gani kwenda kurajis kampuni zake, mali zake kwenye taasisi kama hiyo. Ningeomba Mrajis apatiwe gari kwa haraka, tena gari nzuri ya heshima ambayo itawapa watu imani ya kwenda kufanya *registration* katika taasisi yake. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa hayo machache ningeomba nifikie hapo, mambo ni mengi lakini wakati ni mchache, ahsante sana.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi hii kuichangia ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *(PAC).*

Mhe. Spika, mimi nitaanza na hizi kasoro ndogo ndogo. Kwa kweli hizi si kasoro ndogo ndogo kama zilivyoandikwa, hizi ni kubwa kwa sababu ukiziangalia majumuisho taasisi nyingi zimeidhulumu serikali.

Mhe. Spika, kwanza natoa maelekezo hizi kamati zikichunguza halafu zikitoa maelekezo, wale ambao tunawapa maelekezo wayafuate kwa sababu bila ya kufuata ushauri wetu hatufiki. Sisi tunakwenda pale sio kama askari, sisi tunakwenda kuchunguza, kuelekeza na kuondoa tatizo.

Mhe. Spika, hizi kasoro ndogo ndogo zinakuwa kubwa kwa vipi. Kwanza hili Shamba la Makurunge, lile shamba ni letu lakini eka zimeshachukuliwa si kidogo tumebakishiwa eka 20. Je, Mhe. Waziri hizi zilizochukuliwa tuseme ndio tumewagaia ndugu zetu.

Mhe. Spika, jengine naomba hawa tunaowashauri kwa vyovyote itakavyokuwa waweke *data*, bila ya kuweka *data* siku zote itakuwa hivi hivi. Kama hawana mafunzo tuwaombee mafunzo au maelekezo maalum ya wataalam namna ya kuweka *data* za kuhifadhi fedha za serikali. Lakini tukifanya kazi kiholela siku zote itakuwa tunasema tunampigia gita mbuzi anakula majani.

Mhe. Spika, kwa mfano, pesa za Maktaba bilioni 26 hatuzijui ziko kwenye mazingira ya kutatanisha. Hoja Nam. 57.1.3 Malipo ya Wastaafu hayana marejesho. Ukurasa wa 98 Tsh. 4,356,000/= hatuzijui zimeelekea wapi ziko kwenye mazingira ya kutatanisha. Ukurasa wa 99 Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi hivi vipuri vilivyokuwa havitumiki namuomba Mhe. Waziri tuviuze.

Fedha zenyewe tumeshadhulumiwa tukipata hizi kidogo tutaongezea huko ambako tumedhulumiwa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 107 Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC)* hoja Nam. 400.1 kuhusu malipo ya Tsh. 3,697,000/= pia nazo hatuzijui zimekwenda wapi.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu si mkubwa ni mdogo, hawa watu tuwape mafunzo, taaluma, waweke *data* ili kudhibiti fedha za serikali. Pia tunapokwenda katika taasisi wasituone polisi, sisi si polisi wala *inspector*, sisi tumekwenda pale kuelekeza na kutoa maelekezo yetu wayafuate, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa idhini yako kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya Kamati ya *PAC* ambapo nami ni mjumbe mmoja wapo wa kamati hii.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa watu ambao tumeshuhudia macho kwa macho habari hii hadi kufikia kuandika ripoti hii. Naomba nichangie kwa ujumla ujumla kwa sababu nayakumbuka yale yote ambayo tumeyaona.

Mhe. Spika, kwanza niungane na wenzangu kusema kwamba muda ambao mmetupa kama kamati hautoshi na kanuni ni mali ya Baraza lakini busara za Spika zinahitajika, kuona kwamba *PAC* dhahiri ni tofauti na kamati nyengine kwa utendaji kazi. Kwa hivyo, tunaomba kuona kwamba kamati ya *PAC* inaongezewa muda ili tuweze kupata ufanisi katika kazi zetu. Vyenginevyo nikwambie tu kwamba tutaendelea kuwa na ripoti ambazo haziridhishi na kutakuwa hakuna maendeleo makubwa kwenye nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine niipongeze afisi ya *CAG* kwa kuendelea kutoa ushirikiano na *PAC* na ni dhahiri kwamba wamedhamiria kutuwezesha ili tuweze kufanya vizuri. Kwa maana hiyo, niiombe Afisi ya Baraza la Wawakilishi nayo iungane na afisi ya *CAG* ili watupatie mafunzo angalau kwa nyanja za kuweza kufanya *value for money auditing* na *performance budgeting* kuanzia kipindi kijacho. Kwa sababu kwa hatua kubwa tumetoka sasa kwenye kuangalia risiti, tunakusudia kwenda kuangalia miradi na fedha za wananchi zilivyotumika.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ningelisemea ni daftari la kuhifadhia mali za serikali. Ni kweli kwamba taasisi nyingi za serikali hazina daftari hilo. Mhe. Spika, nitoe pongezi maalum kwa *ZSTC* kwa kutuonesha daftari la kisasa na lenye utaalam wa hali ya juu. Lakini nitoe pongezi rasmi kwa Afisi ya Rais Ikulu wao wamekwenda mbali zaidi kwa kuunda *task force* chini ya Katibu Mkuu kwa ajili ya kusimamia daftari la huduma za serikali.

Sasa ikiwa Afisi ya Rais imeona umuhimu wa jambo hili, nadhani taasisi nyengine za chini yake zitaona umuhimu zaidi. Itakuwa hatuelewi kwamba ikiwa afisi za chini zitadharau suala hili na kuweza kuona kama ni suala la mchezo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lingeligusia ni madeni sugu. Tumeona serikali yetu na taasisi zake zote zilizokabiliwa na madeni sugu. Kama Mwenyekiti wangu alivyosema kwamba tulifanya kikao siku maalum ambacho tulikiita siku ya madeni. Mhe. Spika, siku ya madeni yenyewe wala haikuwa kwenye ratiba ya Baraza lakini tulibuni na kuona kwamba lazima tuwaite watendaji.

Mhe. Spika, nitoe pongezi maalum kwa serikali kwa kuamua kuwalipa *ZSTC* deni lake na kumaliziana. Kwa hivyo, sasa Baraza halina hoja tena kuona kwamba *ZSTC* wanadai. Kwa kuwa *ZSTC* wamelipwa pia hatuoni mantiki kabisa kuona kwamba bado watu walioanguka mikarafuu hawajalipwa fedha zao. Kwa hivyo, watu walioanguka mikarafuu tangu mwaka 1989 mpaka hii leo kwa sababu *ZSTC* tayari wamelipwa fedha zao tungependa kama wawakilishi na watu wale walipwe fedha zao kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la wajibu wa Mhasibu Mkuu wa Serikali. Mbali na majukumu yake Mhasibu Mkuu wa Serikali, lakini ni miongoni mwa majukumu yake kusambaza wahasibu katika idara tofauti za serikali. Wanasambaza wahasibu kulingana na vigezo ambavyo afisi inaona na bila shaka ni vya kitaaluma zaidi. Lakini ningetaka nijue ni kigezo gani ambacho walitumia afisi hii kumhamisha mhasibu aliyeharibu kwa wizi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii chini ya Mradi wa Malaria na wakaamua kumpeleka Idara ya Maktaba kule akenda akachukua milioni 26. Ni vigezo gani ambavyo idara hii walitumia na kuona kwamba bado mhasibu yule anafaa.

Mhe. Spika, hili halikubaliki, mhasibu na mtendaji yeyote wa serikali anayeharibu huyu kazi imemshinda kwa hivyo apumzishwe. Kumchukua mhasibu aliyeiba taasisi moja na kumpeleka katika taasisi nyengine huo ni uzembe na kwa kweli hatuko radhi nao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Waziri anambie ni kigezo gani ambacho walitumia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kumpa uhamisho mhasibu huyu kule akenda akamaliza na Idara ya Maktaba na hadi leo haonekani alipo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, miongoni mwa majukumu yake Idara ya Mhasibu Mkuu ni kuwasambazia watendaji wa taasisi za serikali makasha ya kuhifadhia fedha. Mimi nimekuwa nikijiuliza tunawezaje kununua magari mazuri ya serikali lakini tukashindwa na makasha ya kuhifadhia fedha. Leo ziko taasisi ambazo

fedha zinahifadhiwa ndani ya mikoba ya ukili ni jambo ambalo halikubaliki, ni jambo ambalo utawala bora sijui itafikia vipi. Kwa hivyo, mimi ningeshauri kwamba idara hii wakatafuta makasha haya haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, tumegundua baadhi ya taasisi mfano Halmashauri ya Wilaya ya Chake-Chake barua zipo ambazo wameomba zaidi ya mara mbili, tatu, nne lakini hayapatikani. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa hisani yake suala hili la makasha ya fedha wapatiwe taasisi za serikali, ili fedha iepukane kuhifadhiwa ndani ya mikoba ya ukili au madroo ya meza. Mhe. Spika, suala hili litapunguza kidogo ule uzembe wa upotevu wa fedha na tutakwenda vizuri kwenye utendaji.

Mhe. Spika, jengine ni suala la Shamba la Makurunge. Tumekwenda kuona kule hekta 31,000 za wakati ule, hekta 25,000 amepewa mwekezaji chini ya mkono wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar tulibakiwa na hekta 6,000 sawa na asilimia 20. Hizo hekta zilizobakia wapo pale wafanyakazi Wazanzibari lakini wana hali ngumu sana hawana huduma ya maji, hawana huduma ya afya, hawana huduma ya elimu. Sasa ikiwa kweli tuko *serious* na suala lile basi ningeomba watu hawa wapatiwe huduma muhimu ili kuweza kuwalinda.

Lakini moja ambalo tumegundua Halmashauri ya Bagamoyo imekuwa na malalamiko makubwa kwamba lile eneo lililobakia limekuwa ni chaka la wahalifu. Pale majambazi wanajificha, wauza unga wanajificha. Kwa hivyo, wametwambia ikiwa hamuwezi kuliendeleza basi tupeni lakini msituwekee eneo ambalo sasa majambazi wanajificha. Tumekwenda pale uso kwa uso kuna watu wa ajabu. Mhe. Spika, ningeomba lile eneo ikiwa hatuliwezi basi tuwape wenyewe, lakini tusisababishe kufuga pale majangili na wahuni kwa sababu eti hatuna uwezo.

Mhe. Spika, hili halikubaliki na ningemuomba Mhe. Waziri akalifanyia kazi. Ni eneo zuri ambalo liko ufukweni lakini limetushinda kuliendeleza, hekta 6,000 sawa na asilimia 20 ambazo tumebakishiwa. Katika hekta hizo tayari wananchi wameanza kujenga nyumba wanahamia kwa sababu wanasema kwamba hawajui. Lakini naishukuru Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira wamesema kwamba watalipeleka eneo lile Kizimbani kwa masharti kwamba wenzetu wa Bara wanazingatia matumizi ya ardhi *(land policy).*

Kwa hivyo, wamesema msituombe tu eneo mpaka mtuambie mtatumia kwa ajili gani. Mhe. Spika, hii mimi ningeomba Mhe. Waziri ashughulikie na eneo hili mkazingatia.

Mhe. Spika, namaliza pointi ya mwisho ukaguzi wa Kojani. Ni kweli hali ya Kojani si nzuri ningeomba serikali ikazingatia na tukapata ukaguzi na hatua ya mwisho ya hali ya Kojani ilivyo. Milioni 71 hazikutumika vyema ziko mpaka meza za mizambarau jambo ambalo sio fanicha ambayo serikali hii wanaitaka. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kufikia hapa ikawa tuna afya njema kwa kutekeleza majukumu yetu. Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kunipa nafasi hii nami kutoa mawazo yangu. La tatu niungane mkono na wenzangu na sio kwamba kwa ushawishi au kwa kuhoji kitu fulani.

Mhe. Spika, kamati zinahitaji kuongezwa muda, hili sio Kamati ya *PAC*, wala Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, wala nyenginezo, ni kamati zote. Kwa sababu muda tuliopewa ni mdogo na hii kamati ziongezwe muda kutaisaidia serikali kupata uhakika wa kudhibiti mahesabu yote na mapato ya serikali kutokupotea. Lakini la tatu litalinda heshima ya Baraza kwa kuwa wajumbe waliopo wanafanyakazi zao vizuri kwa kuisaidia serikali ili kupata ufanisi.

Mhe. Spika, la nne ni kusikitika na upotevu wa fedha kwa sababu hili sio la leo na kwa sababu fedha hizi zinapotea kwa kila siku, nina imani wanaopoteza fedha hizi hawachukuliwi hatua. Huwezi mtu ikamwambia leo umefanya makosa nyumbani sikupi chakula, lakini kukamwambia kunywa chai na andazi moja, maana yake ni kumsogeza afanye tena siku nyengine.

Mfano halisi Mhe. Spika, ni kama nyumba ya wilaya ndogo ya Kojani. Mwaka 2008/09 nilikuja nikalieleza hapa Barazani kwamba ujenzi wa fensi na *furniture* zake haifai kwa thamani iliyotolewa. Nashukuru ilikwenda Kamati ya Katiba na Sheria ikaangalia na ikafanyakazi vizuri, wahusika wanamlaumu mwenyekiti kama amewatharau sana maana amewajejea. Mimi nasema hakuwajejea, alifanyakazi yake kwa heshima ya serikali. Tena Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, hongera sana.

Mhe. Spika, lililosikitisha zaidi, tulisema *furniture* haifai na fensi haifai lakini cha kushangaza leo mwenyekiti anatoa ripoti baada ya marekebisho milioni 20 na *point* hazipo, mtu yule keshakosa halafu anaarudishwa tena pale pale, kwani hakuna wakandarasi wengine. Kwa hivyo, itakuwa ni mchezo wa kuchezeana huu.

Mhe. Spika, jengine ambalo ni masikitiko na vichekesho vikubwa. Mtoto unaye ubavuni umembeba, nyumbani uko peke yako umefunga kwa geti nje, lakini halafu ukaambiwa mtoto yule amepotea, ni masikitiko makubwa. Mimi nataka Mhe. Waziri aje anieleze hasa kwa kina, maana juzi katika maswali na majibu

hakupata nafasi ya kunijibu vizuri. Hizi kompyuta zilizopotea, muna walinzi na wafanyakazi zimepoteaje. Waziri juzi alipotujibu kasema labda wafanyakazi walikuwa hawajui. Wafanyakazi vipi.

Leo Mhe. Spika, uko hapo kwenye kiti chako lichukuliwe rungu hapo halafu uje utuambie sijui nini, itakuwa ni vitu vya ajabu sana. Tunataka waziri atufafanulie rasmi na ni hatua gani kwa watendaji wale waliokuwa ndani hatua iliyochukuliwa, sio kurudishwa tena pale kwa sababu itakuwa ni uzembe. Wale wakiachiliwa basi wengine watafanya zaidi ya hilo.

Naomba Mhe. Spika, tuzilinde mali za serikali na tukizilinda mali za serikali basi tutalinda heshima ya viongozi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba watendaji wa serikali au masekta yote ya serikali wawe waaminifu, wasifanye ubabaifu wakawapotezea viongozi wakubwa heshima zao. Tunataka kipindi hiki, kama waziri hatotujibu basi kikao kinachokuja aje atujibu suala la kompyuta jinsi namna zilivyokwenda na hatua zilizochukuliwa.

Mhe. Spika, kwa sababu sina mengi ya kuchangia, kwa hivyo nataka kumalizia hapa, ahsante sana.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuzungumza kwa kifupi sana, kuhusu taarifa hii ya ripoti ya Kamati ya *PAC*. Mhe. Spika, mchango wangu mkubwa utakwenda katika taarifa hii ya upotevu wa pesa za mishahara.

Mhe. Spika, wakati tunatembelea taasisi hii ya Zimamoto zilikopotea hizi fedha, tulipouliza tukaambiwa kwamba walikuwa wafanyakazi bado hawajapewa fedha zao. Kama hivyo ndivyo, basi fedha zimepotea bado mikononi mwa serikali. Zimetoka Hazina zimekwenda kwa mshika fedha wa taasisi hizo, kwa wafanyakazi hazijafika. Sasa tulikuwa tunajiuliza kwa nini hawa wafanyakazi wasipewe haki yao. La msingi hapa ni fedha kufuatiliwa zimepotea vipi. Lakini zitakapokuwa zinafuatiliwa ni kwamba zimepotea kwenye mikono ya serikali. Sasa hawa wafanyakazi wanapewa adhabu kwa kosa ambalo sio lao.

Mhe. Spika, tukashauri sisi kama kamati, ufanywe utaratibu, hawa wafanyakazi walipwe fedha zao, wakati kesi zinaendelea huko huyo mwizi akishikwa atailipa serikali zile fedha. Kwa sababu uzoefu unaonesha Mhe. Spika kwamba hizi fedha hazitapatikana na kama hivyo ndivyo basi hawa ndio wameshadhulumiwa haki yao ya msingi, wamefanyakazi mwezi ule na wanahaki ya kulipwa fedha zao kwa mwezi ule. Mimi nilikuwa nataka nisisitize hilo kwamba hili suala namuomba Mhe. Waziri liangaliwe tena,

adhabu asije akapewa mtu ambaye hastahiki, tutakuwa hatujawatendea haki wafanyakazi hawa.

Jengine Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia suala la *fixed asset registry*. Tumegundua katika kupita kwetu na kamati Mhe. Spika, kwamba hawa wahasibu hawafundishwi jinsi ya kuweka ile *fixed asset registry*, lakini kisingizio ni kwamba hawajapewa utaratibu au *format* na wala hawajapewa hiki. Kwa kupitia kwako nimsifu sana kiongozi wa Zimamoto, wao wana *fixed asset registry* Mhe. Spika, huwezi kuamini. Tukamuuliza wewe umepata wapi hii *format*. Akasema tunafundishwa kama wahasibu.

Pia tukashangaa kwamba taasisi kama Hoteli ya Bwawani, hata lile la kuorodhesha tu kwamba mimi nina viti 5, nina meza 20 na pale hoteli tuna vitanda 50 hawana. Ni taasisi hiyo tunaambiwa ya serikali ijapokuwa haina hodi. Tumeshangazwa sana kwamba hoteli ile ya Bwawani ni taasisi ambayo inajiendesha kibiashara, lakini haina bodi ya kuisimamia. Eti inawajibika kwa Katibu Mkuu nayo ni taasisi ya kuingiza fedha. Kwa hivyo, tungemuomba Mhe. Waziri suala hili aje atuwekee sawa. Inakuwaje katika kipindi chote Bwawani haina orodha hata ile wanaita *inventory* hakuna, basi hata nyuma ya mlango kuweka hapa tuna kiti kimoja, meza mbili na mengineyo, kweli hatuko *serious*.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba hoteli ya Bwawani inatakiwa ifanyiwe marekebisho makubwa. Katika marekebisho hayo basi pia na bodi iwepo, kama tunatambua vizuri kwamba taasisi hii inaingiza fedha lakini tumekuta madeni ambayo Mhe. Spika, tukikutajia hapa utashangaa, eti kikundi cha vijana kinadaiwa. Vijana wamechukuliwa na viongozi kutoka Pemba wamelazwa Bwawani, yule kiongozi badala ya kulipa anasema eti wale vijana ndio wanadaiwa. Sasa masuala kama haya kama kutakuwa na bodi Mhe. Spika, basi hayatajitokeza. Kwa hivyo, tunaomba marekebisho yafanywe kwenye hoteli ile, utaratibu unaoeleweka utumike katika uongozi wa hoteli ile.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako mimi nafahamu umuhimu wa muda, kwa sababu nimeshawahi kukaa hapo. Nataka nizungumzie suala hili la kupotea kwa kompyuta nne katika kipindi cha siku mbili au tatu tofauti, hata mtoto mdogo wa skuli atajiuliza kulikoni. Leo inapotea kompyuta moja, kesho ipotee kompyuta nyengine na keshokutwa inapotea nyengine. Jamani huyu mlinzi yuko wapi, humo ndani ya hizo afisi, maana yake kompyuta zile ziko ndani ya afisi, yule afisa aliyekabidhiwa kompyuta zile hawezi hata kuulizwa basi, hata kutikiswa kidogo hatikiswi Mhe. Spika, eti wameachiwa tu, wanasema tumesharipoti polisi. Hata ile kuwachezesha kwa kuwatoa kitengo hiki na kuwaweka kitengo hiki hakuna ili kuonesha kuwa angalau mko *serious* hakuna.

Mhe. Spika, hapa kuna suala kubwa sana la kujiuliza, namuomba Mhe. Waziri atueleze kwa nini hata ile barua basi ya onyo ya kumuandikia yule *officer resource* wa ile kompyuta hakuandikiwa. Mhe. Spika, nakushukuru sana na ninatunza muda wako, naomba kukaa kitako.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Thuwaybah msaidizi wangu wa kiti hiki pamoja na Mhe. Ali Mzee. Mhe. Ali Denge Makame amenisahihisha, kumbe yeye alitangulia mapema kuomba lakini sio kamati hii ni kamati ya Katiba na Sheria. Nakushukuru Mhe. Ali Denge. Sasa tuwaite Waheshimiwa Mawaziri nadhani wameshajitayarisha.

Nianze kumuita Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kama kuna hoja yoyote. Nakumbuka kuna *policy* imetajwa kwamba haifanyi kazi vizuri, sijui utasema nini.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, kuweza kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kwanza nitaanza na wachangiaji ambao waliochangia zaidi katika suala la muda wa Kamati ya *PAC*.

Mhe. Spika: Ujitahidi haraka haraka kidogo kwa sababu muda umekwenda sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Ahsante, Mhe. Spika, kwa kawaida katika utaratibu wetu wa kazi huwa tunaangalia kwanza bajeti yetu. Katika bajeti yetu ya mwaka 2009/2010 kamati za Baraza zilipangiwa wiki nane nane. Kimsingi katika kumbukumbu zetu tayari kamati zote zimekwishakufanya kazi wiki sita na tumebakiwa na wiki mbili ambazo tutafanyakazi kabla ya kikao cha bajeti.

Kwa hivyo, nilikuwa nawaomba sana wajumbe wa kamati hizi kama kuna wale ambao bado hawajakamilisha kazi zao, basi tunaomba sana katika kipindi kinachokuja tutakapoanza kamati za Baraza waweze kuzitumia vizuri wiki mbili hizi kwa ajili ya kukamilisha kazi zao.

Naomba sana Mhe. Spika, kwa sababu tunajua kwamba kweli kazi zinakuwa ni nyingi na muda wetu unakuwa ni mchache, lakini kutokana na hali ya fedha basi kwa kipindi hiki tumeweza kumudu kuweka hizo wiki sita. Sasa tutajaribu kuangalia kwamba katika bajeti inayokuja Mwenyezi Mungu akitujaalia tukiendelea kuwepo katika Baraza hili basi mfuko ukiendelea kutuna na fungu

letu likiongezwa kwenye Baraza basi tutaangalia uwezekano wa kuongeza hizi wiki nyengine za kuweza kufanyakazi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba kutokana na muda wako kuwa mchache basi nitazungumza kidogo hili suala la wizi ambao umejitokeza. Mhe. Spika, tumezisikia hoja za wajumbe na nawaomba sana kwamba suala hili tuachiwe tulifanyie kazi. Tunategemea katika kikao kinachokuja basi tutaweza kutoa ufafanuzi kwa sababu kwa kuwa wizi umetokezea itabidi sasa tuanze kuchukua hatua za karibu zaidi. Mhe. Spika, kama ulivyonitaka kuwa afisi yangu iwe karibu zaidi na jeshi la polisi ili kuona kwamba hivi vitendo vya wizi tunajaribu kuvipiga vita. Mhe. Spika, nakushukuru kwa hilo ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Ahsante Mhe. Spika, kwanza naipongeza hii kamati ya *PAC* kwa kazi nzuri walioifanya na kuweza kugundua mambo mengi kabisa ambayo kusema kweli yanahitaji kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, mimi nina hoja tatu. Kwanza ni hoja ya wizi wa kompyuta katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, kamati ilipokwenda imekuta kwamba afisi ilichukua hatua ya kuandika barua polisi kuelezea habari ya wizi. Nadhani kilichokuwa kifuatie pale ni polisi kuja afisini na kuwachukua wale ambao wamehusika na wizi huu kwa ajili ya kuisaidia polisi, hilo halikufanyika. Hata hivyo, mimi nimekuwa nikimtuma afisa kutoka wizarani kufuatilia polisi juu ya suala hili, mwisho wenyewe afisi ya mrajis imeandika barua baada ya kuwataka wafanye hivyo kwa ajili ya kukumbushia sana suala hili.

Suala hili Mhe. Spika, bado liko polisi na ninasema napokea agizo la kamati kwamba lazima suala hili linapomalizika basi wapewe taarifa kamili kwamba limemalizika vipi na kama ni wizi hatua zichukuliwe. Nakubali hilo agizo kabisa Mhe. Spika. Vile vile napokea agizo la pili lililotolewa na kamati ya *PAC* juu ya tabia ya kujikopesha pesa huu sio uaminifu. Nakubali kabisa kuwa sio uaminifu na hiyo tabia itabidi waiwache kabisa. Hiyo ndio hoja ya pili.

Hoja ya tatu ni kuwa Mrajis Mkuu wa Serikali hana gari. Mhe. Spika, ni kweli Mrajis Mkuu wa Serikali hana gari na gari lake liko katika hali mbaya sana na sio rahisi kuweza kulitengeneza, ni afadhali kununua gari mpya. Tumeomba katika mgao wa kwanza ule, lakini kwa bahati magari yalikuwa yameshamalizika. Kwa hivyo, tumewekwa katika *bench* kusubiri haya magari mengine yatakapoletwa ili Mrajis tumpatie na yeye gari.

Mhe. Spika, bahati mbaya afisi yangu haina gari nyingi kiasi hicho kama angalau ningeweza kumchotea moja nikampa yeye, hili ndio tatizo ambalo

nimelipata katika afisi yangu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, na hili nalo nalipokea kutoka kwa kamati na tutaendelea kushirikiana.

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa niaba yao napokea pongezi walizozitoa kamati hii ya *PAC* kwa kushirikiana nao vizuri na kwa sababu wenyewe wapo watakuwa yote wameyasikia bila shaka. Kwa hivyo, ni hatua nzuri na wao kidogo kidogo wanapopata uwezo huwa wanawasaidia angalau kuwapa mafunzo mafupi mafupi kidogo. Hili nadhani Afisi ya Mdhibiti itaendelea kutoa mafunzo kwa ajili ya kamati hii. Kamati hii Mhe. Spika, inasaidia sana serikali katika kuona kuwa fedha zinatumika kwa mujibu wa kanuni za matumizi ya serikali. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kueleza machache, mbali ya yale yaliyoelezwa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi na mengine yatagusa maeneo ambayo Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi atakayoyaleta.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kupokea ushauri ambao umekuja kutokana na fedha ambazo mara nyingi huwa zinaibiwa. Ni kweli suala hili limeshatokea karibu vikosi viwili au vitatu. Kitu kimoja ambacho kimeleta matatizo ni kuwa fedha zinaibiwa na wapiganaji wanakosa mishahara, kwa hivyo hapa nini kifanyike.

Mhe. Spika, pamoja na masuala yote hayo, fedha zinapoibiwa kwa mujibu wa taratibu za utawala, waliohusika ni kufanya uchunguzi na kikosi cha polisi ndicho ambacho kinatakiwa kifanye uchunguzi huo. Wakati wameshaanza kuingia huko, basi inabidi sisi tungoje matokeo ambayo yatatolewa na kikosi ambacho kimepewa kufanya kazi hiyo.

Je, wale ambao hawajalipwa mishahara yao, ni watendaji ambao wamefanya kazi na wanastahili kupata mshahara, lakini mpaka inafika wakati huo pesa zinaibiwa basi mshahara hawana. Hili ni jambo ambalo inabidi kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kulitafutia mbinu ya kulitatua tatizo hili. Kwa wale ambao wamefanyakazi basi mishahara yao wapewe na wale waliohusika na kesi hii kuichunguza basi waendelee kuchunguza kama sheria inavyoelekeza.

Jengine ni suala la Kojani. Ukaguzi ulifanywa na kamati na kutolewa ripoti ya mapungufu. Afisi ilifuatilia na kumtaka mkandarasi azikamilishe samani zilizopungua zenye thamani ya milioni 21. Pia afisi ilimleta Mkandarasi na kumuandikia barua rasmi ya kukamilisha vifaa hivyo na nakala ya barua hiyo ilipelekwa katika kamati ya *PAC*. Hatimaye pia Mkandarasi alikamilisha vifaa

vyote isipokuwa meza nne tu na hizo aliahidi kuzikamilisha wakati wowote kuanzia sasa.

Aidha, kwa sababu Mkandarasi huyo bado anadai fedha zake katika afisi, kwa hivyo suala hili litakwenda kwa kudaiana na kudai. Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kupata wasaa huu na nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na kamati yake kwa kazi nzuri kabisa. Kama nafikiri alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora, kwamba kwa kweli kazi wanazofanya zinatusaidia sisi tunaosimamia matumizi ya fedha kuona kuwa fedha hizi zinatumika ipasavyo.

Vile vile nimuunge mkono Mhe. Mwakilishi wa Magogoni kwamba kazi ya kamati hii sio kama *inspector* kuwa anakwenda kutisha, hapana. Wao wanatimiza wajibu wao na sisi tunawapa kila msaada. Nafikiri Mhe. Spika, hata kamati haitutaki mawaziri kwenda kwenye kamati yao na kufanya kazi, kwa sababu wanataka wazi kabisa wakutane na watendaji wamalizane nao. Hata kuna mambo mengine Mhe. Spika, ndio tunayasikia hapa, hata hatuyajui kwa sababu wanataka watu-*cash by surprise* na ni vizuri.

Kwa hivyo, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora, kwa kweli baadhi ya mambo wameweka sawa, kwa hivyo mimi sitaki kuyarejea.

Naomba kusisitiza kwamba sio lengo la serikali kuwatesa hao walioibiwa mishahara. Haja yetu na wao wafaidike kama wametoka jasho basi walipwe ipasavyo. Tutajitahidi ili kuona kwamba zile kesi zinaharakishwa upesi upesi na haki zao zilipwe. Au kama alivyoshauri ndugu yangu Mhe. Mazrui kwamba walipwe halafu mengine yafuate. Huo ushauri tumeusikia kama walivyokwishasema wenzangu tutayazingatia kwa pamoja.

Mhe. Spika, Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu alitaka kujua kuhusu mnada wa hoteli ya Bwawani. Nafikiri juzi Mhe. Ramadhan Nyonje alikuwepo tulipopitisha sheria hapa ya kulinda mali za serikali kutopigwa mnada kiholela kama hivi. Nafikiri alikuwepo na matarajio yetu ni kuwa sheria hii itazidi kunusuru na mali nyengine za serikali. Sio jambo jema mtu anadai milioni 5 au milioni 2, basi mtu anakwenda serikalini anahangaishwa na mtendaji kisha anakwenda mahakamani inapigwa mnada. Kwa hivyo, hii serikali nafikiri itafilisiwa kila kitu itakuwa haina *asset* yoyote.

Pia hatuna lengo la kuwatesa wanaoidai serikali, tumeweka utaratibu anayedai serikali afuate utaratibu gani. Sasa ni kweli kwamba kuna deni la mchele na lipo kwa siku nyingi sana kwenye kampuni moja ya kule Thailand. Kwa hivyo, serikali tunajitahidi ili tukutane na huyu bwana anayetudai, maana yake tuna wasi wasi kama hawa wanaofuatilia pengine ni matapeli wa kati na kati na hiyo kampuni kama imeshafilisika. Lakini kama kweli tunawasiliana nao wajitokeze upesi upesi ili tuweze kukaa nao na tuone vipi tunaweza kulimaliza jambo hili na liweze kumalizika.

Kwa hivyo, hili suala mahakama kweli waliamuru mnada mmoja iuzwe Bwawani, lakini kwa busara ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu suala hilo likaondoshwa na tunazidi kutafuta uwezekano kuzungumza na huyo muhusika.

Wakaguzi wa ndani Mhe. Spika, nao wameguswa kuwa hawafanyi kazi zao ipasavyo. Kwa kiwango fulani nakubaliana nao kweli kwa sababu kama makosa yapo na yanabainika mpaka kamati inakwenda na inayaona wao wanakuwa wapi. Huu ni ushauri mzuri ambao tumepewa na tutakaa pamoja na taasisi yangu hii ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ambao ndio dhamana ya hawa wahasibu pamoja na wakaguzi wake, ili tuone hasa nini chanzo cha matatizo na vipi tuweze kurekebisha.

Mhe. Spika, sehemu nyingi tumepewa ushauri, ukiondoa zile kesi maalum kama Mhe. Hija Hassan Hija ile ya mhasibu yule wa malaria. Hiyo ni kesi maalum kama ni mhasibu kaburunda. Kwa kweli tunamuhamisha bila ya kumchukulia hatua au bila ya kuchunguza huko sio kuwajibika. Ni lazima tuchunguze tuone matatizo yako wapi na yeye tumuwajibishe. Mimi nakubaliana na ushauri wake. Kumuondoa tu mtu keshafanya madudu ukamtoa huku na kumpeleka huku, nafikiri sio jambo jema. Kwa hivyo, ushauri wake tumeusikia na tutaufanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba ushauri mwingi walioutoa Waheshimiwa Wajumbe, basi Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wamenisaidia. Kwa hivyo, tutakaa pamoja ili kuona kwamba haya masuala tunayashughulikia ipasavyo. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Pengine kamati hii imetoa hoja kubwa sana ambayo imekuwa inazisumbua kamati zote, kwamba afisi hii ya Baraza haina gari za kamati. Sasa sijui kama utasema kitu ambapo nitashukuru sana juu ya hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa sasa tutaziomba wizara zote za serikali, kwa pale wanapopangiwa ratiba au kama

vile tunavyokwenda hivi sasa basi kuandaa mpango mzuri tu kwa Waheshimiwa Wajumbe wasipate tabu waweze kupata magari ambayo yanaweza kupita mpaka matopeni, wakati tunajiandaa na huo mpango Mhe. Spika, ambao umeniuliza moja kwa moja.

Mnajua Mhe. Spika, ana kitu, mimi na yeye tuna mazungumzo yetu ya kupatiwa mabasi mapya na ya kisasa hapa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, hilo Mhe. Spika, limo njiani na tunalifanyia kazi. Ninaamini baadae tukishayapata hayo mabasi basi asaakheri mambo haya yatakaa sawa, ahsante.

Mhe. Spika: Hiyo inaitwa kuchomekeza mambo. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, na baadae Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niende kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Fatma Ferej ambaye ametaka kujua kuhusu wizi wa mishahara ya shilingi milioni 4.8 katika hospitali ya Micheweni.

Kweli Mhe. Spika, fedha hizo ziliibiwa na sio zilipotea, ziliibiwa na watuhumiwa walikamatwa na baadae walifikishwa mahakamani na hukumu yao waliachiwa huru kwa kuambiwa kwamba umekosekana ushahidi. Sasa baadhi ya wafanyakazi wetu wa Hospitali ya Micheweni wamekosa mishahara hiyo. Kwa hivyo, tutawasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kuona vipi tutaweza kulitatua tatizo hili.

Mhe. Spika, Mhe. Haji Mkema alitaka kujua kuhusu milioni 61 za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zilizopotea. Mhe. Spika, hizi fedha hazijapotea. Hizi ni fedha kutoka *UNICEF* na mradi wa *FAST*. Huu ni mradi maalum tumepewa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tumezitumia vizuri na malipo yake yamekwenda vizuri na zile *original documents* zimekwenda *UNICEF*.

Sasa *copy* ndio tunazo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hapa ndio palipotokea kutokufahamiana. *UNICEF* wanataka *documents* zilizokuwa *original* kabisa na wale wakaguzi na wao wanazitaka zile zile, sisi tuna-*copy*. Sasa kutokufahamiana hapa ndio kutokea hilo tatizo. Sisi tunaendelea vizuri na *UNICEF* wanatupa fedha tunafanyakazi zetu vizuri na mpaka juzi tumewapa fedha za kununua chanjo, hakuna tatizo lolote kuhusu fedha hizi. Kwa sababu kungetokea tatizo basi *UNICEF* wasingetupa fedha zao wala kungekuwa hakuna mahusiano mazuri.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija, Dk. Mwinyihaji amekwishaeleza, kuwa kweli huyo alikuwa ni mfanyakazi wa kitengo cha malaria na hakudumu.

Wenyewe Wizara ya Fedha na Uchumi wakamuhamisha. Kwanza alitoka Wizara ya Elimu huyo, akaletwa kwenye mradi wa malaria, akatoka mradi wa malaria akapelekwa maktaba, tena milioni 26 sijui zimetokea vipi Kwa hivyo, uhamisho wa wahasibu sio kazi yetu, isipokuwa ni kazi ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Lakini Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi ameelezA vizuri na wala sitaki kuharibu mambo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, baada ya haya nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini kabla sijajibu hoja hizi naomba uniruhusu kidogo japo kwa dakika mbili au tatu kuzungumzia kidogo mazungumzo ambayo yanazungumzwa mitaani, hapa Waheshimiwa Wawakilishi wapo wote pamoja na waandishi wa habari wapo, jambo hili linaipaka matope serikali. Kwa kweli hiki ni chombo ambacho ni muhimu sana kwa jamii. Kwa hiyo, nakuomba uniruhusu dakika mbili au tatu nitoe ufafanuzi.

Mhe. Spika, kuna gazeti ambalo lilichapisha la Mwananchi na likaweka picha ukurasa wa mbele kabisa kusema Waziri wa Elimu "Apiga Marufuku Mabaibui". Kwa kweli jambo hili nilifikiria limekwisha kwa sababu yule mwandishi mwenyewe alinipigia simu na kuniahidi kwamba kwenye gazeti lake angeomba radhi, kwa sababu aliniomba radhi na kuniambia samahani Mheshimiwa kwa usumbufu ulioupata.

Lakini napenda kuweka sawa kidogo kwamba serikali haijapiga marufuku uvaaji wa mabaibui na hilo ni moja. Isipokuwa serikali ilichopiga marufuku ni walimu kuvaa kanzu ambazo hazina mikono, kanzu zilizo juu ya magoti na zenye kubana au kuvaa kanzu ambayo inaonesha mwili na hiyo ndiyo sahihi. Kwa kweli hili lilikuwa limeshakwisha, sasa tena masika yameshaanza basi tunapakwa matope na ikifika Mei na Juni itakuwa tayari nimeshasafika na *Inshaallah* itakuwa hakuna matatizo *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, niende kwenye hoja moja kwa moja kuna masuala mawili ya kimsingi. Kwanza kuna matatizo ya wahasibu wetu hawa wanatuletea matatizo na wala sikujua kama mhasibu huyu aliyepelekwa kwenye Mradi wa Malaria alitokea Wizara ya Elimu na halafu akarudi huku.

Kwa sababu suala la uhasibu kabisa na wala mimi kama waziri sina uwezo wa kumhamisha na unapotaka kuchukua hatua hiyo inabidi usome sura ambayo inayoanza kwa tafsiri yake si rahisi kueleweka. Sasa bado suala hili naomba Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi atusaidie, kwa kweli wapo wahasibu ambao

wanatuletea hasara kubwa sana ndani ya serikali yetu na suala hili liko polisi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nashauri nadhani tunapojadili ripoti za kamati kama taratibu zinaruhusu siku kama ya leo, basi Mkuu wa Polisi Zanzibar pamoja na timu yake wangekuwepe, kwa sababu mambo ya wizi haya yanahusiana na masuala ya wizi wa fedha, wangekuwepo nao wakasikia, hata kama mawaziri pamoja na viongozi wengine tupo na tunasikia. Lakini polisi moja kwa moja nadhani wangekuwepo wenyewe wangesikia *(Makofi)*.

Kwa kweli nashukuru kila ukiwapelekea taarifa kwamba mmefikia hatua gani, wanasema ndio tumo. Sasa kesi hii kwa mfano, tulikuwa na Naibu Waziri wetu Mwalim Mbarouk kutoka Mgogoni kule wakati ule Waziri wa Elimu Mhe. Ramadhan Mapuri, basi huwa anatuita sisi watendaji wakati mwengine na mimi nilikuwa Naibu Mkurugenzi.

Sasa humwambia tuko mbioni, basi yeye husema nyinyi Wakurugenzi hamfiki mbio zenu hizi. Kwa hivyo, na hili sasa nadhani ni kweli umefika wakati hizi mbio iwekwe ile *tape* ya kugusa. Mhe. Spika, suala hili hatuwezi kulipeleka au Polisi hawawezi kulipeleka Mahakamani, kwa sababu mtuhumiwa hajakamatwa. Kutokana na hali hiyo, naliomba sana Jeshi la Polisi pamoja na mimi nachukua agizo hili kwamba nitamwita Mkuu wa Jeshi la Polisi na kumwambia sasa masuala yamefika Barazani, basi jitahidi kwa sababu fedha za serikali hata kama ni shilingi moja ni fedha ya mwananchi.

Jambo la pili Mhe. Spika, nakiri vile vile kwamba kuna matatizo ya fedha za *retention* kupatiwa. Kwa kweli tumejaribu kuzungumza na wenzetu wa Wizara ya Fedha na hivi juzi tu Mhe. Waziri mwenyewe nilizungumza naye, kwa sababu kuna mengine ya masuala ya fedha kwamba kuna haja ya kuletewa moja kwa moja kwenye wizara hasa yale yanayohusiana na *Skill Development Levy*. Kwa kweli ameniahidi kuwa waziri suala hili atachukua hatua na kuanzia mwezi huu *Inshaallah* natarajia hizo fedha zitakuja. Kwa hivyo, ni kweli pamoja na hayo lakini sio kama hatupati fedha moja kwa moja, isipokuwa zinakuja fedha pale wizarani na halafu sisi tunagawana kama vile Idara ya Nyaraka ipewe kiasi gani na nyengine ipewe kiasi gani. Tatizo mara fedha zinakuwa kidogo tu lakini fedha zinakuja isipokuwa hazitoshelezi mahitaji.

Kweli hali ya makumbusho yetu yanahitaji matengenezo makubwa, pamoja na hayo tayari tumeshaanza kuyafanyia kazi hivi sasa.

Mhe. Spika, nakushukuru *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kujibu hoja za Ripoti ya Kamati ya *PAC*. Kabla ya yote niungane na wenzangu kumpongeza Mwenyekiti pamoja na wajumbe wake wote kwa jumla kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa kweli kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba mimi sina matatizo na ripoti kama hizi nadhani zinatusaidia serikali. Hivyo, nawapongeza sana kwa kazi yao nzuri waliyoifanya *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mimi ninalo moja kuliko yote nalo ni kuhusu Makurunge. Kwa kweli imeelezwa hapa shamba la Makurunge kuna sehemu ambayo imechukuliwa. Kwa hivyo, napenda kusema hivi kwanza shamba hili sisi tulipewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuliendeleza na tuliendeleza, lakini ilifika wakati mambo hayakuwa mazuri.

Sasa kama sikosei kiasi ya miaka miwili au mitatu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitaka sehemu baada ya kumpata mwekezaji. Kwa kweli iliiomba rasmi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ilikubali kwamba hiyo sehemu waliyoomba wamekubaliwa. Kwa hivyo, sisi tumebaki na sehemu ambayo aliyoitaja Mwenyekiti wa Kamati. Vile vile ni kweli sehemu hiyo hivi sasa tumeipa Chuo cha Kizimbani kuiendeleza.

Mhe. Spika, kabla ya hapo napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba kutokana na hali ilivyokuwa ya Makurunge, serikali iliunda kamati wajumbe kutoka Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo na kufanya kazi vizuri sana na kuleta ripoti serikalini, hiyo ripoti kwa jumla imo katika kufanyiwa kazi hivi.

Miongoni mwa hayo yaliyopendekezwa kuwa tuweze kuipa taasisi yoyote ya serikali kama vile Chuo cha Kizimbani, kwa maana ya kwamba sio serikali moja kwa moja basi huenda tukapata Hatimiliki. Kwa hivyo, suala la Hatimiliki tumo kulishughulikia lakini mpaka hivi sasa bado hatujaipata. Lakini tumo katika mazungumzo na serikali ya mkoa pamoja na wilaya kuweza kutupatia hii Hatimiliki.

Kuhusiana na suala la uvamizi pia tumezungumza kama alivyosema Mwenyekiti kwamba tumezungumza na Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo pamoja na Makurunge kwa jumla. Hivi sasa wamo katika hatua serikali yake ya wilaya na mkoa kwa ajili ya kuwaondoa hawa wavamizi. Mhe. Spika, ni kweli wapo wavamizi kwa sababu mimi mwenyewe nilikwenda ambao ni wengi tu, yaani wamevamia kwa makaazi hasa pamoja na familia zao, kupika na kupakua. Kwa hivyo, Serikali ya Wilaya pamoja na Mkoa zinachukua hatua za kuwaondosha watu hao. Kutokana na hali hiyo wizara yangu itashirikiana na Wakuu wa Wilaya na Mkoa ili kuhakikisha hawa wavamizi wanaondoka. *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nafikiri nimejaribu kujibu hoja za Mwenyekiti kuhusu shamba la Makurunge. Kwa kweli wakati tulipokwenda kule walikuwa na kilio kikubwa ambacho wanastahiki, yaani hawa usafiri wala chochote. Kwa hivyo, tumeanza kuwapa mapikipiki na hivi sasa wakati wowote kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuweza kutupatia angalau gari moja ya kuweza kusaidia usafiri kutoka kule mpaka Bagamoyo.

Vile vile walipiga kelele kwamba hawana Kituo cha Afya, ambapo ni kweli kwa hiyo, tunajaribu kuzungumza na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kuangalia kuna uwezekano gani wa kuwa na kituo, ikiwa hapana budi basi angalau wawe na huduma ya kwanza. Lakini maombi au malalamiko yao yanastahiki kusikilizwa *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa ufupi haya ni majibu ya hoja za Mwenyekiti wa Kamati hii kama nilivyoeleze hapo awali.

Nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ (Kny. Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji): Mhe. Spika, nimeshajibu swali mengi.

Mhe. Spika: Kama limeshajibiwa hakuna zaidi basi labda nikushukuru tu. Nyongeza Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, Mhe. Kaimu Waziri nafikiri alijaribu kuweka ufafanuzi wa baadhi ya mambo, isipokuwa nataka kuongezea tu, kwenye Hoteli ya Bwawani.

Mhe. Spika, ni kweli waheshimiwa wengi wamelalamika kuhusu utendaji wa kazi katika Hoteli ya Bwawani, hata Mhe. Thuwaybah Edington Kisassi akauliza kwamba, he! basi hata kumbukumbu za *register* ya viti na nini hamna tofauti na afisi nyengine na hii mali ya serikali?

Kwa kweli Hoteli ya Bwawani Mhe. Spika, ni katika hoteli yetu moja ambazo tunazienzi ili tuwe nazo na tumeamua hasa isiuzwe. Kwa sababu wamekuja watu wanataka kununua au kuwekeza lakini tumeamua kwa makusudi ibaki kama chombo chetu cha serikali, kwa huduma zetu za serikali na kwa mambo mengine yetu. Kwa mantiki hiyo, lazima kiwe chombo chenye utendaji mzuri na kama kioo kwetu.

Sasa tunakubali ushauri mzuri sana tena naomba niinukuu hasa ile sentensi kwamba, “Hoteli ya Bwawani ifanyiwe mapitio makubwa”. Sijui Mheshimiwa

gani alisema hilo lakini kwa kweli tunaunga mkono sana sentensi hii. Naahidi Mhe. Spika, kama serikali tutashirikiana kuona kweli Hoteli ya Bwawani tunaipitia, tunairekebisha iwe kama kioo kwa taifa letu.

Mhe. Spika, naomba hapa hapa nichomekee, umenifundisha wewe Mhe. Spika na si jambo baya, kwamba kulikuwa na suala kubwa sana lile la *asset register* na habari ya muongozo kwamba haujatolewa.

Nimepata *breaking news* hapa kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mwenyewe Mkurugenzi Said Hussein, ananambia kwamba muongozo tayari umeshatolewa kwa taasisi zote na zimeshasambazwa nakala za *asset register* kwa Makatibu Wakuu wote, ili lianze na hivi karibuni wataanza semina kwa afisi zote Pemba kwa kuelimisha na hapa matayarisho ya Unguja yameanza. Walianza semina Pemba na sasa wanakuja Unguja. Nimepata masahihisho kidogo ni Kamishna wa Mitaji ya Umma. Naomba radhi kwa hilo.

Kwa hivyo, kazi Mhe. Spika, ya *asset register* imeanza na tunasisitiza tu, kwa Waheshimiwa Makatibu Wakuu watusaidie ili kuona kwamba yale mambo yaliyozungumzwa na mwongozo yanakwenda vizuri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwanza napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, lakini kulikuwa na suala moja tu ambalo limezungumzwa na Mhe. Haji Mkema Haji lililozungumzia juu ya suala la kodi ya ardhi ya wawekezaji ambayo kwa ripoti hii ni jumla ya US$ 1,554,000 na 91.80.

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kupitia *ZRB* tunaendelea na jitihada za kuwasiliana na hawa wanaodaiwa ili waendelee kulipa deni hili.

Mhe. Spika, mafanikio yamekuwa yakionekana na napenda kulithibitishia Baraza lako Tukufu wakati wa bajeti ukifika lugha itakuwa nyengine, huyo Mhe. Haji Mkema Haji asiwe na wasi wasi kwa wakati huo kuja kuzuia shilingi kwa jambo hilo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa idhini yako ni kwamba sisi tulikuwa na suala moja tu kwa upande wetu, moja lilikuwa la jumla ambalo Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameshalijibu kwa ujumla kwa wizara zote.

Suala jengine alilizungumza Mhe. Asha Moh'd Hilal, yeye alizungumzia vipuri lakini hasa ilikuwa ni magari machakavu ya wizara yetu. Sisi kama wizara tatizo hili tunaliona na hili tatizo liko katika Idara ya Uhakikimali ambayo vile

vile iko Wizara ya Fedha. Kama kutakuwa na utaratibu wowote wa magari haya kuuzwa sisi tuko tayari ila tu vile vifaa vyengine kama vya ujenzi na utunzaji wa barabara hatuko tayari kuviuza kutokana na hali halisi iliyopo. Kwa sababu kwa upande wa magari tayari tumepata magari ambayo yanatuwezesha kufanya kazi zetu kwa sasa.

Kwa hivyo, wakati wowote ule ambapo Wizara ya Fedha itakuwa tayari katika kuuza magari tunapokea maombi hayo Mhe. Spika. ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. spika, sisi hatujatajwa kwa kheri wala shari, inaonekana mambo yetu yanakwenda vizuri. Sekta ya habari inafanya kazi yake, kamera kama unavyoziona Mhe. Spika, katika Baraza lako mpya zile, zinaitwa *HDV* maana yake *High Definition TV*.

Tumetajwa sehemu moja tu katika ripoti hii ambayo ni Sauti ya Tanzania Zanzibar, nalo lile deni linaendelea kufuatiliwa na nadhani Wajumbe wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali watakuwa wameona kwamba kuna tofauti ya lile deni linaanza kulipwa kidogo kidogo. Kwa hivyo, hilo ni dogo tu.

Lakini Mhe. Spika, mimi naomba niipongeze sana kamati hii kwa sababu imevunja rekodi ya Baraza. Mimi nilikuwa mjumbe wa kamati hii mwaka 2005 mpaka mwezi wa Febuari, 2006 tulipoteuliwa katika nafasi hizi tulizokuwanazo sasa hivi. Wakati ule tukiwa wajumbe wa kamati tulikuwa tunaongozwa na kiongozi shupavu Mhe. Abass Juma Muhunzi akiwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Mimi nilishangazwa sana mwaka 2006 sisi tulikuwa tunaangalia hesabu za 1998/99, sasa leo nawapongeza sana kwamba wamevunja rekodi ya Baraza wako kwenye mwaka 2008/2009. Hii inaonesha utendaji mzuri.

Mhe. Spika, mara nyingi huwa tunazungumzia mapungufu lakini kwa kweli kazi inayofanyika katika ripoti hii ni kubwa sana. Wakati ule tunafuatilia mwaka 1998/99 ilikuwa ni kichekesho kwa sababu hata wale waliokuwa wametutangulia katika Baraza hili walikuwa tayari wameshaondoka na wao hawapo, kwa sababu wameingia mwaka 2000–2005, lakini sasa hivi tunaweza kuona kwamba hesabu za karibu zinafuatiliwa na huu ni usimamizi mzuri na sisi tutajitahidi kwa upande wetu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tunashukuru, nafikiri tumemaliza wizara zote, tunawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, basi tumkaribishe mtoa hoja Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Karibu.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali): Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya

Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako tukufu ambao kwa njia moja au nyengine, kwa kuchangia kwa mdomo au kwa kutulia kimya kutafakari yale yanayozungumzwa. Wameisaidia kuijadili Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, napenda kuwatambua waliopata nafasi kwa sababu ya muda wako kuwa mchache, kuichangia kwa mdomo ripoti yetu na naomba niwatambue kwa kuwataja ni hawa wafuatao:-

Mhe. Haji Mkema Haji
Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
Mhe. Asha Moh'd Hilal
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Omar Ali Jadi na
Mhe. Thuwaybah Edington Kisassi.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru sana mawaziri wetu wote ambao wamejitahidi sana kujibu angalau baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza katika ripoti yetu na kutoa ufafanuzi ambao ulikuwa unahitajika hapa na pale. Napenda niwashukuru kwa kuwataja majina yao nao ili niwatambue nikianza na:-

1. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi
2. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora
3. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ
4. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa BLM Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi
5. Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii
6. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
7. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira
8. Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji ambaye maelezo yalitolewa kwa niaba na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na vile vile Mhe. Waziri Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi, wote walijaribu kujibu hoja zilizojitokeza katika wizara hiyo.
9. Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi
10. Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu namshukuru pia ndugu yangu
11. Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Napenda nithibitishe tu kwamba kimya kile cha kutokutajwa ndani ya ripoti ni kheri juu yake kwamba mambo yao yanakwenda vizuri (*Makofi).*

Mhe. Spika, nawashukuru sana hasa mawaziri kwa kutoa ufafanuzi juu ya ripoti yetu. Lakini niwaombe jambo moja kwamba mwisho wa ripoti hii ndio mwanzo wa ripoti nyengine ambayo itakuja kujadiliwa ndani ya Baraza hili.

Kwa hivyo, ninawaomba sana kwa kupitia *Accounting Officers* ambao wanao ndani ya wizara zao, yaipitie kila wizara kwa inapohusika ile ripoti kwa ukamilifu kama ilivyo ndani ya kitabu chetu, ili yale ambayo yameshauriwa na kamati waweze kuyafanyia kazi *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya hayo napenda kukushukuru ahsante *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji kama ripoti hii mumeipokea na kuikubali, wale waliopokea ripoti hii na kuikubali wanyanyue mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ripoti ifanyiwe kazi na serikali kwa maeneo yote ambayo yamo ndani ya ripoti hiyo na taarifa ya utekelezaji wake irudishwe kwenye Baraza hili *(Makofi).* Tunashukuru sana.

Mhe. Haji Omar Kheir Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala karibu sana, lakini uzungumze kwa kifupi bila ya kwenda kwenye ripoti ambayo ni ndefu kidogo, tena ufundi huo anao na ninamuamini sana *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi hii kuwepo hapa na kuja kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya utendaji wa shughuli za serikali.

Kwa sababu umenitahadharisha juu ya muda na ripoti yangu imekusanya kurasa 29 haitayumkinika Mhe. Spika kusema vyenginevyo. Kwa kuwa tunataka kuokoa muda, basi ningeomba nisende kwenye ripoti, isipokuwa niseme yale ambayo ninayakumbuka kwenye ripoti yetu.

Vile vile niwaomba Waheshimiwa Wajumbe waiangalie ripoti yetu kwenye ukurasa wa 111mpaka 149.

Mhe. Spika, naomba niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Haji Omar Kheir	-	Mwenyekiti,
2. Mhe. Haji Mkema Haji	-	Makamo Mwenyekiti,
3. Mhe. Zahra Ali Hamad	-	Mjumbe,
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	-	Mjumbe,
5. Mhe. Najma Khalfan Juma	-	Mjumbe,
6. Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	-	Mjumbe,
7. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	-	Mjumbe,
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe,
9. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mjumbe,
10. Mhe. Fatma Abdalla Tamim	-	Mjumbe,
11. Ndugu Nasra Awadh Salmin	-	Katibu na
12. Ndugu Abdalla Ali Shauri	-	Katibu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nawapongeza watendaji wa wizara zote nne ambacho ziko chini ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala nazo ni hizi zifuatazo:-

1. Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,
2. Wizara ya Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi,
3. Wizara na Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora na
4. Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema sitajitendea haki kama nitarukia rukia bila ya kuisoma ripoti kamili. Lakini kwa sababu wajumbe wamekuwa macho kitabu hiki kwa muda mrefu bila ya shaka watakuwa wamekipitia na kukisoma vizuri na hasa zile wizara zinazohusika.

Kwa kuwa Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala naomba nigusie mambo machache ambayo Kamati ya *PAC* hivi karibuni iliyokuwa kwenye meza na mjadala katika Baraza hili imeeleza mambo mbali mbali, ambayo sisi kama kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tunahisi yangefaa yakaangaliwa na kuzingatiwa sana na serikali *(Makofi)*.

Kwanza suala zima la manunuzi na ugavi katika taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa kweli tumeona jambo hilo lina mapungufu makubwa sana, kwa sababu baadhi ya taasisi zimekuwa hazifuati taratibu na kuweza kulishughulikia jambo hilo ipasavyo. Wanaohusika katika kitabu watajiona wenyewe na maana yangu ni kwamba kwenye bajeti ijayo, basi wizara na taasisi husika zitakuja hapa zikiwa zimelirekebisha jambo hilo.

Jambo la pili la jumla ambalo nataka niliseme la baadhi ya taasisi kutokufika mbele ya kamati bila ya sababu za msingi. Hivyo, ni vizuri taasisi zikaelewa

kwamba jambo la kutokufika kwenye kamati ni kukimbia na kukwepa majukumu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, hapa nataka nisema zaidi kwa watendaji wakuu wa serikali hasa Makatibu Wakuu, baadhi ya Makatibu Wakuu wamekuwa wanapoitwa na kamati hutokezewa na safari nyengine ambazo sisi tunazihisi si za msingi sana kuliko kuja kuripoti juu ya jambo ambalo limefanyiwa kazi katika wizara ile *(Makofi)*.

Suala jengine la jumla ambalo limezungumzwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya suala la *furniture* na ujenzi wa Afisi ya Wilaya Ndogo Kojani. Kwa kweli hili kamati yangu kila mwaka imekuwa inaliripoti, lakini hatua hazichukuliwi.

Namshukuru Mhe. Waziri wakati alipokuwa akitoa ufafanuzi alisema kwamba kulikuwa na baadhi ya vifaa havikukamilika, lakini hivi sasa vimekamilika.

Siku moja nilimsikia mtu anasema kwamba unaweza kuwa na *degree*, lakini *degree* yenyewe ya kinyozi, nikisema kinyozi nyote mnafahamu. Pamoja

na kwamba *furniture* ambazo amezisema zimekamilishwa, lakini hivyo tujiulize kuna benchi lililochongwa kwa mfenesi lenye thamani ya laki tatu? Sasa tunachozungumzia hapa thamani ya *furniture* ambazo zimewekwa, thamani ya ujenzi ambao umejengwa na fedha ambazo zimetumika. Kwa hivyo, hapa *value for money* haipo ndicho ambacho kimekusudiwa na kamati yangu pamoja na Kamati ya *PAC*.

Mhe. Spika, kwa sababu umenitaka niokoe muda nimesema kwamba wajumbe wanalo kabrasha hili naomba waangalie kwenye ukurasa wa 111 mpaka 149. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, umenisaidia sana kwa kuokoa muda ili tuweze kumudu kumaliza shughuli zetu hizi kwa muda mchache ambao tunao kabla hatujamuomba Mhe. Waziri Kiongozi kuja kutoa hotuba ya ufungaji wa mkutano huu.

Waheshimiwa Wajumbe kabla kuchangia ripoti hii nilitangulia kusema mapema kwamba tunao wageni wa michezo ambao wameingia hapa nchini tangu jana saa za laasiri na katika ratiba yao kwa kuwa tunaendelea na shughuli hizi wametaka kuja kuwasalimia wenyeji wao, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nafasi nilizonazo hapa ni chache kidogo kwa hiyo ningewaomba ingawa kuna mvua wale ambao tumemaliza shughuli zao sasa watupatie nafasi kidogo ili wale wageni wetu nao wapate nafasi ya kuingia. Wabakie wale

ambao wanahusika na ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambao ni Wizara ya Tawala za Mikoa, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora, Wizara ya Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Baraza la Mapinduzi.

Hao ndio wanaohusiana na ripoti hii wao ningewaomba watendaji wakabaki na wengine niwaombe sana kwamba siwafukuzi napenda sana musikie kinachoendelea, lakini kwa ufinyu wa nafasi humu ndani basi ningewaomba sana na mvua imetukubalia kupungua kidogo watoke taratibu watupatie nafasi na wageni wetu waje tuwatambulishe kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wanakuja kuwasalimia asubuhi hii. Tufanye hiyo kazi watendaji tusaidieni kufanya hiyo kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, mimi ningesaidia kidogo kwa sababu inaonekana hawa wote ndio sasa hapa wangebaki wale Makatibu na wengine wangepanda juu ili wale wageni wetu waingie humu ndani.

Mhe. Spika: Ni katika kurekebisha hili suala ili liende vizuri. Wakati huo huo wale wageni watayarishwe waje wasimame tuwatambulishe, lakini bila ya kupoteza muda basi tuanze na mchango na watakapoingia tutasita kidogo ili baadae tuwatambulishe wageni wetu.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwanza kabla ya yote nimuombe Mwenyezi Mungu anilinde na anipe fasaha ya kuzungumza ili niichangie vyema ripoti hii na ifahamike.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze wana kamati hii jinsi ya ratiba zao na taratibu zao nyingi walizokuwa wameziandika ndani ya buku letu hili.

Mhe. Spika, nakuja kwenye ukurasa wa 123 kifungu cha 5 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar naomba kunukuu. “Ilitoa mafunzo kwa wajumbe na watendaji wa Tume ya Uchaguzi juu ya utatuzi wa migogoro katika masuala ya uchaguzi na uandikishaji wa wapiga kura”.

Mhe. Spika, kwa kuwa mara nyingi tunapofanya chaguzi zetu huwa kunatokea migogoro na mivutano mbali mbali kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi kunakuwa na mikakati, kwa kuwa tukimaliza uchaguzi kwa kila mjumbe aliyeshiriki akubali matokeo. Lakini miongoni mwetu baada ya kumaliza uchaguzi baadhi ya wengine wanakuwa wanakataa matokeo. Kwa hivyo, kunakuwa na utata kwa wanachama wetu wanakuwa roho juu, kwa hiyo kwa kuwa wakati unakaribia na tume hapa imetoa walimu kwa kuchukua mafunzo

zaidi. Ningeiomba tume ikatoa wanafunzi wazuri zaidi ili kutoa taaluma katika masuala haya ya uchaguzi yanayotarajiwa hivi karibuni. Mhe. Spika, hiyo itasaidia kuepusha matatizo mbali mbali yanayoweza yakajitokeza baada ya kumaliza uchaguzi huo.

Mhe. Spika, jengine kwa nini hatusikii kuchukuliwa hatua za kisheria na kupata adhabu kwa wale waliokuwa wanaleta migogoro ili isitokee tena. Mhe. Spika, hapo ningemuomba Mhe. Waziri akija apatolee ufafanuzi zaidi tukaweza kujua tujipange vipi kwa kipindi kinachokuja.

Mhe. Spika, pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa wizara hii kwa juhudi zake kubwa anazozichukua za kuimarisha haki za binadamu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, sasa nije katika ukurasa wa 125 Idara ya Kukabiliana na Maafa kifungu cha 6 naomba kunukuu. “Iliendelea kuandaa Sera ya Taifa ya Kukabiliana na Maafa kwa kukusanya maoni na michango kutoka kwa Kamati za Kukabiliana na Maafa za Mikoa yote mitano, Wilaya 10 na Shehia 200 za Zanzibar”.

Mhe. Spika, kitu ambacho kinanichanganya kwa kuwa wizara hii imefanya hivyo na mimi ndani ya jimbo langu nilitokea na maafa tarehe 9 Disemba, 2009 juu ya upepo baadhi ya wananchi wangu zaidi ya nyumba 74 ziliezuka, nyengine zikapasuka na kuta kuanguka. Kwa hivyo, Idara ya Maafa ikanitembelea na kuwaona wananchi wangu kwa kuwapa matumaini ya kuwafariji. Sisi viongozi wa jimbo tukapewa changamoto akiwemo Mbunge na Mwakilishi tukajaribu kuwasaidia wananchi wale, lakini mpaka leo kimya kimekuwa kirefu idara hii haijatoa jibu lolote. Kwa hivyo, mimi ningeiomba idara hii ikija hapa inieleze ili wananchi wasikie kuna utaratibu gani wa kusaidiwa kabla ya kuchanganya masika wajijue wanatengeneza vipi nyumba hizo ambazo ziko wazi na nyengine zimefunikwa mabati.

Mhe. Spika, baada ya matokeo haya ya maafa na kutembelewa na baadhi ya viongozi wa kitaifa akiwemo mpaka Mhe. Rais utakuta mpaka sasa hivi masuala haya bado hayajapatiwa ufumbuzi. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akija hapa anifahamishe na wananchi wangu wajisikie wamefaidika vipi na Idara hii ya Maafa.

Mhe. Spika, kwa kuwa idara hii ina mengi na muda tuliokuwa nao ni mdogo kwa hivyo mimi naipongeza pamoja na wananchi wangu na kuwaomba viongozi wenzangu tuipitishe ripoti hii bila ya pingamizi yoyote. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nafikiri wale wageni sasa wapo tayari Waheshimiwa Wajumbe naona wageni wetu wako tayari na kabla hatujaendelea na mjadala wa ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala basi nichukue nafasi hii Waheshimiwa Wajumbe kwanza kukushukuruni kukubali kuwapokea wageni wetu na waje kuwasalimia. Wageni wetu hawa utakuta wanatoka nchi mbali mbali lakini hawa wanatoka Arusha na hawa ni wageni wa timu yetu rafiki ya *Wazee Sports Club* ya Arusha. Sasa kwa nini watatoka nchi mbali mbali?

Kwa sababu wakaazi wa Arusha wote wageni na wenyeji wameamua kutengeneza club hii ya Wazee Sports Club ambayo imechukua wageni mbali mbali ambao kuna Mahakama pale ya Kimataifa pale Mjini Arusha nao pia kwa ukarimu na utamaduni wetu wa Tanzania basi hawakuwekwa kando wamekubaliwa kuingia katika *club* hiyo ya wazee, ili baada ya kazi zao ngumu wote kwa ujumla wapate nafasi kwa mujibu wa ratiba zao wawe wanacheza pamoja jambo ambalo nalo huwa linadumisha umoja si katika Tanzania lakini pia nchi za Afrika. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe muwapongeze wageni hao ambao leo wamefika hapa na nitawaita mmoja mmoja ili muweze kumuona na mtakuwa mnampongeza kama kawaida yetu. Nianze kwa kuwataja majina na kuwakaribisha.

1. Ndg. Danford Mkumilwa huyu ndiye mwenyekiti anatoka nchini Tanzania. Tunamshukuru sana na karibu sana ndugu mwenyekiti.
2. Bwana Ali Mamuya, na yeye pia anatoka Tanzania.
3. Ndg. Marrin Foreis, huyu anatoka Cameroon.
4. Ndg. Maick Taylor, huyu anatoka Tanzania.
5. Ndg. Wimme Mgonja, kutoka Tanzania.
6. Ndg. Harith Vin, anatoka Liberia.
7. Dk. Makando, anatoka Tanzania.
8. Ndg. Asa Atogo, kutoka Cameroon.
9. Ndg. Mboya, kutoka Tanzania.
10. Ndg. Claud Petego, kutoka Cameroon.

Hiyo ndio orodha ambayo nimeipata sasa wale wengine ambao sikuwataja kwenye orodha hii ningeomba wasimame kwa pamoja ili nao waonekane kama wapo. Karibuni sana nyote tunakushukuruni kuja kuwasalimia ndugu zetu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiwa kazini na wanasema kwamba karibuni sana mjisikie mko nyumbani na hii vile vile ni nyumba yenu na msiwe na wasi wasi pamoja na mvua lakini ratiba itaendelea kama ilivyopangwa. Karibuni sana wageni wetu na ahsanteni sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, na mimi naungana na wewe kwa kutoa shukurani zetu za dhati kabisa kwa wageni wetu waliotufikia hapa kwenye ukumbi huu, lakini nataka kusema kwamba tutawafunga tu usiwe na wasi wasi wowote.

Mhe. Spika, kwa kuendelea kuchangia nitachangia katika vikosi vyetu vya SMZ hasa kikosi cha KMKM. Kwanza niwape pongezi sana kikosi hiki kwa jitihada zao nzuri sana walizozifanya katika kuendeleza jengo lile la hospitali ambalo lina mambo ya kisasa.

Mhe. Spika, hapa ningeomba kidogo serikali nayo iwasaidie na itoe nguvu zao zote ili kuweza kumaliza na ile ghorofa iliyobakia wakati vifaa vitakapokuja vya kisasa waweze kupata nafasi nzuri ya kuviweka. Lakusikitisha ni kwamba watakosa wataalamu waliokuwa wenye uwezo wa udaktari kutokana na hali ya mishahara.

Mhe. Spika, hali ya mishahara kwa kweli haijaridhisha kwa madaktari wao. Hivi karibuni kuna taarifa kwamba kuna kijana mmoja wamemsomesha vizuri lakini baada ya kupata shilingi laki saba akaona bora akae huko kwenye laki saba kuliko kurudi kwenye mshahara mdogo. Suala hili mimi naomba tuliangalie kila siku tunaambiwa marekebisho ya mishahara lakini bado hatujawa makini kuweza kurekebisha ili watu wetu wasitukimbie.

Mhe. Spika, kidogo naomba unipe nafasi ya kutoa mfano. Kwa mfano, kama Hospitali ya Mnazi Mmoja tusipoangalia wataalamu wetu watatukimbia kutokana na hii hali ya kila siku ya marekebisho ya mishahara mpaka hivi sasa hayajapata ufumbuzi wake hili ni moja ambalo litaleta athari kubwa sana. Mhe. Spika, sasa hivi ukiangalia hata zile *uniform* zao hazikidhi haja kutokana na hali ilivyo, utakuta wengine wanatimilia na wengine hawatimilii na hili ni suala ambalo tulitizame kwa kina kabisa ili kuweza kusaidia askari wetu wawe makini kama sheria inavyotuelekeza.

Mhe. Spika, nikiendelea katika Kikosi cha JKU kikosi hiki nacho nimewasifu sana kutokana na jitihada zao. Nataka nipewe taarifa rasmi kuhusu habari ya hili shamba la mboga mboga kwa muda mrefu sana hatujapata kujua liko vipi na limekwama wapi ili serikali iweze kuwasaidia. Kwa sababu kuweza kulima mboga ni sababu moja ya kuondoa umaskini na kupata ajira kwa wale ambao wanakwenda kujitolea na kuweza kujikimu na maisha yao.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba nenda kwenye ripoti mambo mengine yaweke wakati wa bajeti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, la mwisho ni kuhusu Idara ya Maafa sijui kuna aina gani ya watu wanaowajibika kupewa misaada kati ya wanaoangukia na minazi na wale wanaopata majanga ya moto. Hapa ningeomba na hili nisaidiwe pia na hizi Halmashauri tumesema na wao wapewe hizi sheria ili waweze kukusanya vizuri mapato yao.

Mhe. Spika, kwa hayo machache kwa kuokoa wakati wako naomba niunge mkono ripoti hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake wote, pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wa wizara hizi pamoja na Makatibu wao na watendaji wao wote kwa kazi nzuri walizozifanya kutuletea ripoti hii sahihi.

Mhe. Spika, mimi nitazungumza machache sana. Kwanza nitazungumzia suala la Idara ya Walemavu. Mhe. Spika, katika dunia hivi sasa tunaamini kwamba hakuna jambo linalopigiwa kelele kama watu wenye ulemavu, lakini naipongeza serikali kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba inaweka idara hii ili wenyewe wajipange na waendelee kufuatilia mambo yao mbali mbali kwa ajili ya maslahi yao na taifa.

Mhe. Spika, moja ambalo nataka kulichangia kwanza ni kwamba watendaji wa idara walikutana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini/Magharibi, hii ina maana kwamba kukutana kwao huko walikaa wakafikiria jinsi ya shida wanazozipata walemavu kwa njia moja au nyengine. Mhe. Spika, kwa sababu tunapata taarifa mara walemavu wamebakwa, mara limetokea hili, kwa hivyo wamepanga mkakati mzuri wa kukutana na kuliondoa hilo. Kwa hivyo, naipongeza sana.

Mhe. Spika, pili ni kwamba iliandaa kikao muhimu sana hapa Zanzibar kwa ajili ya kutafuta mbinu na mambo ya misaada ili kuimarisha idara hii na watu wake. Jengine ni kwamba ilikutana na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa ajili ya kufuatilia ujenzi wa kituo cha watoto yatima au wenye mazingira magumu kinachotaka kujengwa huko Kitogani. Nawapongeza sana kwa kuliangalia hilo hasa tukizingatia kwamba watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanataka kusaidiwa, na shirika hili litakapoweza kujenga kituo hicho basi naamini wananchi wetu watafaidika na hilo.

Mhe. Spika, nikija kwenye Baraza la Manispaa la Zanzibar ni kwamba mimi natoka katika Mkoa huu wa Mjini/Magharibi, nataka nilipongeze Baraza la Manispaa kwa kazi nzuri ambayo hivi sasa wanaifanya. Mhe. Spika, tulikuwa na kilio katika Baraza hili katika bajeti iliyopita kwenye machinjio ya kuku, wenzetu wamefuatilia na wameona utekelezaji unavyokwenda vizuri, kwa hivyo naipongeza kamati kuhakikisha kwamba maeneo yanayotoa huduma za jamii ziwe safi.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba tuiangalie michirizi yetu ya maji machafu hivi sasa tunaamini mvua za misika zimeshaanza, kwa hiyo watu wetu wengi wako roho juu lakini naishukuru serikali kupitia Baraza la Manispaa kwa kazi nzuri inayotekelezwa ya kutoa huduma mbali mbali. Mhe. Spika, mimi ombi langu ni kwamba juzi nimeuliza swali hapa linalohusu michirizi inayomwaga maji Kizingo, bahati mbaya kamati haikutembelea sehemu hiyo na haikupata fursa hiyo, lakini mimi kwa kuwa mitaro hii inayotoka Kwahani inanigusa namuomba sana Mhe. Waziri na watendaji wake waufuatilie mtaro ule kwa sababu hivi sasa hali ni mbaya sana. Mhe. Spika, mtaro ule umebomoka na umo katika mazingira magumu kwa hiyo naomba tuuwahi mapema tusije tukaharibikiwa huko mbele.

Mhe. Spika, jengine ambalo nitasema kwa ufupi sana ni kwamba hakuna jambo la wivu kuliko maendeleo, nikimuona Mhe. Fatma Fereji amefanya jambo zuri sana basi na mimi nitataka nimshinde yeye huku ndiko kuigana kimaendeleo. Mhe. Spika, natoa pongezi za dhati katika Halmashauri zetu zote kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini natoa shukurani za pekee kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kati Zanzibar.

Mhe. Spika, Katibu wa Halmashauri hii kwa muda mfupi aliokuwepo hivi sasa maendeleo yamepatikana labda mara mia zaidi. Kwa hivyo, nampongeza Mkurugenzi kupitia kwa watendaji wake kwa kukusanya mapato mengi ambayo yamevuka lengo na sio vibaya Halmashauri nyengine ziige. Mhe. Spika, kwa ufupi hivi sasa Halmashauri imenunua gari kama shilingi milioni kumi na nne, taarifa hiyo ninayo kamili. Pongezi hizo azipokee Mkurugenzi pamoja na watendaji wake wote wa Wilaya ya Kati.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa mimi mara nyingi huzungumzia suala la vikosi. Vikosi ni roho ya nchi na askari mara zote huwa ndiye mlengwa wa mwanzo kukulinda wewe, mimi niliyesimama hapa na mpaka anayetusikiliza huko nje na bila ya askari huna usalama. Mhe. Spika, katika safari zetu zote tunazotembea likikutokea tatizo utamfuta askari akusaidie. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana utaratibu ambao unajitokeza kwa bahati mbaya askari ni dhamana, askari anatakiwa yeye mwenyewe ajilinde, ailinde silaha yake, akilinde kinachomfaa. Kwa hivyo, taratibu ambazo zimejitokeza huko nyuma

za kupotea mishahara ovyo Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri na Makamanda wetu wa Vikosi wasikubali utaratibu huu ukajitokeza tena, kwa sababu askari sawa sawa na mwanafunzi yeyote darasani. Mwanafunzi kama zinapita kalamu zinagaiwa hivi akikosa basi atakasirika, kumbe askari naye huko anakotoka kwa vile mimi natokea kwenye jeshi najua vizuri, nikikosa kiwi katika kikosi changu basi anaona kama kakoseshwa shilingi milioni moja, kwa jambo dogo tu.

Kwa hivyo, tulitizame hilo dogo tulione kubwa lakini mshahara ndio ndio jambo la mwisho. Hivyo namuomba sana Mhe. Waziri hili aliangalie na makamanda wetu wawe makini kabisa katika kuhakikisha haki za askari, malipo yao yanakuja kwa wakati ili wafanye kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa heshima kabisa naunga mkono ripoti hii, namuunga mkono mwenyekiti wa kamati na wajumbe wake wote na wale wote walioshiriki. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe, sasa nimkaribishe Mhe. Zahra Ali Hamad na baadae aje Mhe. Ramadhan Nyonje. Lakini kabla Mhe. Zahra hajaanza, wageni wetu wanataka kufanya kitu kimoja kidogo ambacho ruhusa nimeshatoa kutokana na yale maeneo ambayo naruhusika, wanataka kuchukua picha wakiona kwamba sisi tuko kazini. Sasa watendaji watawafahamisha wakae wapi wanaweza kupiga picha isiyokuwa katika maeneo ya ndani humu, alama zake zimo na hiyo ambayo wataweza kuchukua. Hata wale wengine bila ya kuleta usumbufu wanaweza wakapiga picha kutokea hapa nyuma.

Sawa, basi kazi hiyo watendaji saidieni msije mkaona mnamurikwa murikwa sana ni picha ambazo wageni wetu wanataka wapige wakiona kwamba tuko kazini. Mhe. Zahra karibu.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuchangia ripoti hii. Mimi kwa kweli sitokuwa na mengi kwa sababu ni mjumbe katika kamati hii na kama ambavyo imezungumzwa kwamba ripoti yetu ni refu sana na katika kitabu hiki ripoti hii imeanza ukurasa wa 111 mpaka 148. Nataka kuzungumza kitu kimoja tu ambacho hakikuji-*appear* Mhe. Spika, katika ripoti yetu na kwa kweli ni jambo muhimu.

Mhe. Spika, katika ziara zetu za kamati tulitembelea katika shamba la JKU, nadhani hata Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ndiye aliyetaka kujua kwa sababu humu katika ripoti yetu haiku-*appear* .

Kama tunavyokumbuka mradi huu umeanza zamani kidogo na ni mradi ambao wenzetu wa Misri wanatuchangia, sasa Wamisri tayari wametimiza jukumu lao

la wataalamu na vifaa, jukumu lililobakia ni letu sisi kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba mradi ule unafanikiwa.

Katika bajeti yetu hii ya mwaka 2009/2010 mradi ule ulikadiriwa upewe shilingi milioni mia tano, lakini mpaka juzi mzunguko wetu wa mwisho wa ripoti yetu tumekuta bado una pesa kidogo ambazo hazifikii hata nusu ni shilingi milioni mia moja na tisini ambazo wenzetu hawa wamepewa.

Sasa Mhe. Spika, mradi wa mboga mboga ni mkombozi kwetu, kama ambavyo…

Mhe. Spika: Wageni wanatuaga wanatoka taratibu, kwa hivyo, tunaweza tukapata nafasi kama watatoka kwa pamoja basi tunaweza tukawapongeza wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wetu tunawashukuru sana, Mhe. Zahra endelea.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Ahsante Mhe. Spika, nilikuwa nasema kwamba mradi huu wa mboga mboga ni mkombozi kwetu. Kama tunavyojua kuwa Zanzibar tuna mahoteli mengi ya kitalii ambayo yanahitaji mboga, lakini sisi wenyewe Wazanzibari pia tunahitaji Mhe. Spika, mboga mboga kwa ajili ya kulinda afya zetu. Sasa mimi nadhani abebwae siku zote hujikaza, tujikaze. Wenzetu wametimiza jukumu lao na sisi hichi ambacho tuliahidi kukitoa ili mradi huu umalizike Mhe. Spika, naiomba sana serikali ihakikishe kama hawa wenzetu wa JKU wanatiliwa hizi pesa ili huu mradi ukamilike.

Pia tulitembelea na tuliona yale matunda ambayo tayari yamejitokeza. Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni mashahidi ile kidogo tu waliyoanza kuzalisha wameleta hapa na kuanza kuuza. Sasa mimi nadhani kama mradi huu ukifanikiwa basi baada ya sisi kuagiza mboga kutoka Bara sasa tutachukua Zanzibar na kupeleka Bara. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nitakuwa na mchango mdogo tu. Mimi binafsi nimepokea kwa masikitiko sana taarifa ya kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, nilikuwa nikimsikiliza Mwenyekiti wa Kamati hii alipokuwa akiwasilisha taarifa ya kamati kwa kweli isingekidhi haja kutokana na ukubwa wa kamati yenyewe. Lakini maelezo yake ni mazuri, nimeyafahamu, isipokuwa kuna moja ambalo mimi mwenzenu limenikasirisha, halikunifurahisha, halikunipendezesha na linanisikitisha sana.

Mhe. Spika, Mwenyekiti alipokuwa anawasilisha ripoti yake alieleza tabia ya watendaji wakuu wa serikali kutokuhudhuria katika kamati zetu za Baraza. Mhe. Spika, hii maana yake nini? Hii maana yake ni kwamba Baraza lako hili linadharauliwa na hiki si chombo cha kudharauliwa na mtu mwengine yeyote. Sisi tuliomo ndani ya Baraza tumechaguliwa na wananchi kwa kura nyingi sana ajabu, kuja kuwawakilisha. Kazi za kamati ni miongoni mwa kazi na majukumu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kazi zile zinafanywa na wawakilishi waliokuwa wanaitwa *backbenchers,* mle haingii waziri, Mkuu wa Mkoa, lakini kama tutamtaka waziri kuingia tukimuhitaji tunamualika. Lakini Makatibu Wakuu watendaji ni lazima wahudhurie katika kazi hizi za kamati.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kuona kwamba baadhi ya Makatibu Wakuu hawafiki, na hii sio leo tu, tumezungumza mara nyingi lakini tatizo liko wapi? Tatizo ni kwamba Baraza letu hili Mhe. Spika, sijui Maalim Abdalla atataka niseme vipi, lakini nasema hatuko *serious.* Hatuko *serious* kwa sababu lazima tukunje uso, ni kwamba sheria zipo *Act Nam. 4* ipo, Baraza lina haki au kamati ina haki ya kumwita mtu yeyote kuja mbele ya kamati na kutoa ushahidi na kueleza mambo mengine yakihitajika. Sasa hawa watendaji tunaowahitaji kwenye kamati lakini hawafiki.

Nafikiri Mhe. Spika, katika kipindi kijacho mwaka 2011 pengine, hii tabia ya kuleana leana tuiache. Kwa sababu hii yote ni kuleana leana tu na sijui tunawalea kwa kubembeleza kitu gani. Sisi tunafanya wajibu wetu lakini kuna tabia ambayo baadhi ya Makatibu Wakuu wanasema wao ndio serikali na serikali, bila ya sisi hapa hakuna Katibu Mkuu, hakuna waziri. Sasa hili ni jambo Mhe. Spika, linakasirisha sana, iweje mtu unamwita katika kamati asije aone kazi yake ni muhimu sana kuliko shughuli nyengine.

Mhe. Spika, hili ni kosa na ni tatizo kubwa, naomba sheria zitumike na Katiba itumike, tuwashughulikie makatibu wetu kama hawa wasiowajibika. Kwa sababu nasema huko ni kutokuwajibika, laitani ingekuwa tunajua umuhimu wa chaombo hiki basi tusingefika kiasi hicho.

Mhe. Spika, hapa naomba unisaidie mimi kwa sababu mimi najua, naomba ulisaidie Baraza na wananchi, na kule kwenye ripoti hii katika kifungu cha Baraza la Wawakilishi kumetajwa ujenzi wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi. Hapa naomba watakaokuja ku-*wind up* wanisaidie na wawasaidie wananchi wapate kuelewa, ni lini hasa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi litakabidhiwa? Sisi tunazo nukuu nukuu tunapata kwenye vikao vyetu, mnatueleza lakini wananchi wanauliza ni lini Baraza hili jipya la fahari litafunguliwa?

Sasa iwavyo vyovyote, kama maelezo yako kama tulivyoelezana au kinyume cha hivyo mzidishe *speed* ili kuona kwamba na sisi ambao tulikuwa tunasogeza mawe tunaliwahi Baraza hili.

Mhe. Spika, nataka kutoa mfano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Spika, Pius Msekwa ndiye aliyekuwa *engineer* mkuu, ndiye aliyehamasisha, ameshajihisha, amefanya kila kitu lakini matokeo yake hakuliingia na hakulikalia. Sasa nina wasi wasi isije ikafika kiasi hicho ikawa tunapiga debe, kofi lakini tusije tukaingia. Nataka sote tulionje Baraza jipya kwa fahari na kujivunia.

Mhe. Spika, katika ripoti hii kwenye Mrajisi Mkuu wa Serikali. Ripoti imesema kwamba kuna vyeti 5,128 vya kuzaliwa, ripoti imeandika vimegawiwa, mimi sijui niseme vimegawiwa au vimetolewa. Lakini katika vyeti hivyo, vyeti 4653 vilitolewa kwa wahusika na vyeti 475 bado vipo wilayani. Hivi vyeti vimetolewa kwa mujibu wa wilaya zote nne zilizoko Pemba. Sasa najiiuliza, hawa waliokuwa hawajachukua vyeti vyao bado viko wilayani wamekufa, hawapo au vipi?

Kwa sababu vyeti 475 kama watoto waliozailiwa ni vingi, lakini kama vimetolewa vyenginevyo sielewi, kuna wengine wanabadilisha kwa sababu vimechakaa, kuna vyengine vimetafunwa na panya, lakini iwavyo vyovyote vile Mhe. Spika, basi vyeti 475 vilivyoko wilayani vifanyiwe utaratibu. Nadhani wahusika wanasikia hivyo vyeti vifanyiwe utaratibu vikachukuliwe, vyenginevyo ni kwamba watakoseshwa haki yao kama watoto, kama watu wazima. Nilikuwa nasisitiza kwamba vyeti bado viko wilayani lakini vikachukuliwe.

Mhe. Spika, kwa sababu nimetanguliza kwamba sitakuwa na mchango mkubwa na kwa sababu ya buku hili ni kubwa na mna ripoti nzito. Lakini la mwisho nauliza, hivi hizi taarifa zetu za kamati Makatibu Wakuu wanazo? Au zinaishia hapa tu kwa mawaziri na wawakilishi? Kwa sababu kuna mambo ambayo yametolewa mapendekezo na maoni ya kamati ni mambo muhimu sana ya kuzingatia, lakini na maoni ya Mhe. Haji Omar Kheir kwa sababu hakuyasoma kuna mambo nime-*notice* hapa ni muhimu sana kiasi cha kwamba wenzetu wangekuwa wanapata haya basi wangeyafanyia kazi.

Kwa mfano Mhe. Spika, niruhusu kwa vile Mhe. Haji Omar hakusoma kutokana na muda naomba uniruhusu nisome kidogo kwenye changamoto na mapendekezo ya kamati, ukurasa wa 139 *bullet* ya tatu. Inasema, "ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi na utaalamu mdogo wa madaktari. Mfano; hakuna '*pathologist'* wa kufanyia uchunguzi miili ya marehemu iliyotokana na vifo visivyokuwa vya kawaida. Aidha, baadhi ya wataalamu mara nyingi hawatoi

ushahidi mahkamani hususan madaktari kwenye kesi za shambulio". Hii ni hatari Mhe. Spika, kama daktari unatakiwa ukatoe ushahidi na wewe huendi maana yake nini?

Sasa ndio nauliza hivi vitabu wanavyo, wanapata hizi taarifa? Mimi nadhani Mhe. Spika, kila mmoja awajibike kwa mujibu wa nafasi yake. Baada ya hayo nasema nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Juma Duni Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kidogo nichangie ripoti ya kamati hii. Mimi nilitaka kugusia kuna ukurasa wa 115, 116, 117 ni ndefu kidogo mpaka 119 siendi kote, lakini inaonekana ni maelezo marefu kuhusu Afrika Mashariki. Naona wenzangu wengi waliosimama kuchangia hawajaligusa suala hili.

Mhe. Spika, kwanza naomba kukushukuru kwamba mimi na Mhe. Salmin Awadh kikao kilichopita tulipata nafasi tukashiriki mkutano mmoja kule Arusha. Mkutano ule kidogo ulikuwa wa kitaalamu mambo ya hatimiliki na mambo ya ufumbuzi na mengineyo. Sasa labda mwenzangu alikuwa na uzoefu lakini mimi ilikuwa ni mara yangu ya kwanza.

Tumesafiri tumefika pale sasa nawatafuta wataalamu wetu ambao watusaidie kutueleza mambo ya kitaalamu ili sisi tukifika pale tushiriki hakuna. Nikamuuliza mwenzangu shughuli hii iko chini ya wizara gani kule kwetu? Akasema yeye anadhani ni Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, wengine wakasema nadhani Ikulu, kulikuwa na taarifa fulani tunazipata nikasema nipige simu lakini namba ya Wizara ya Biashara ikawa nimeisahau. Nilikuwa huko miaka mingi, waziri siijui nambari yake ya simu.

Kwa ufupi Mhe. Spika, hapa kuna kitu muhimu sana kwa Zanzibar na kinaonekana bado hakijatulia usimamizi wake. Kuna mambo yaliyokuwa si ya muungano na mambo ambayo yana maslahi na Zanzibar. Bahati nzuri Mhe. Spika, katika kikao kile ilikuwa zile sheria zinazojadiliwa bahati nzuri sheria na sisi tumeshatunga, na ikawa bahati kwamba ile sheria yetu ni nzuri zaidi kuliko hata ile ya Bara. Lakini nawatafuta wataalamu wa kutusaidia siwaoni, Mhe. Salmin shahidi pale.

Sasa niliporudi hapa nakumbuka nilikutana mahala fulani na wewe Mhe. Spika, nikakwambia nakushukuru tumekwenda kule lakini turipoti wapi baada ya kurudi? Turipoti kwako au wizara gani? Katika kuuliza uliza nikaambiwa suala hili linashughulikiwa na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapiunduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi.

Mhe. Spika, katika kutafuta kwangu nikaambiwa kijana mmoja pale anaitwa Mselem bahati nzuri namjua nilikuwa naye wakati nikiwa Wizara ya Mipango. Amekuwa *expert* anajua tangu mambo haya yalivyoanza lakini kishastaafu, nauliza yuko wapi naambiwa yuko *Chamber of Commence*, nikapiga eeh! mama yangu wee! Yuko *Chamber of Commence?* Nani badala yake, sina hakika labda Mhe. Waziri atatusaidia.

Ukisoma hii ripoti kuna miradi mengine inaonekana imeshaingizwa katika miradi ya Afrika Mashariki. Sasa silaumu pengine ni kwa sababu sina taarifa za kutosha. Nani anasimamia shughuli hizi na zinahitaji zijulikane kwa sababu mambo mengine yanahusu wenzetu Bara lakini mengine yanatuhusu sisi, na sisi huwa wa kwanza kulalamika kwamba hatupati haki zetu lakini jamani tumejiandaa vipi?

Kuna mahali hapa ripoti inasema Mhe. Spika, kuharakishwa uundwaji wa kamati ya wataalamu wa kuzingatia vikwazo na changamoto zinazokwisha kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki. Wataalamu wetu tunao, tumewatayarisha, wapo?

Mimi siwezi kumuagiza Rais kwamba basi teuwa wizara inayohusu mambo haya kwa sababu hiyo ni shughuli yake, lakini nadhani tunahitaji kuzikusanya shughuli hizi zikajulikana zinaratibiwa wapi. Kila siku zitakavyokwenda shughuli hizi ni muhimu kwetu na zitatuathiri. Ukitizama humu kunakuja sarafu ya pamoja, kunakuja paspoti ya pamoja, mambo ya forodha ambayo yanatuathiri sana. Sasa tukiyaacha yana *hang* yanaweza kutupa shida sana Mhe. Spika.

Mimi sina hakika lakini siajabu keshokutwa nikaambiwa niende tena kuhudhuria mkutano, ninapata tabu sana kwamba sina pahali pa kuuliza na sina pahali pa kujibu. Mhe. Spika, nisichukue muda wako mrefu *my concern* ni kwamba suala hili linahitaji mahali liratibiwe na liwe na usimamizi na tuweze kujenga wataalamu watakaokuwa na uwezo, tusiogope hata tukiwa na mmoja kwanza, tutajiimarisha, hakuna hata mmoja hapa aliyezaliwa anajua alifu, bee, tee ya quraani. Lakini sote leo hapa *Alhamdulillah* tunasali tunaijua.

Sasa tukianza kutakuwa na mmoja, atakuja wa pili, watatu, tutaanza kuwa na *unit*, idara, mwisho tutakuwa na mkurugenzi anashughulika na mambo ya Zanzibar kwenye Afrika Mashariki. Lakini hali tuliyo sasa naona kidogo hakuna mshiko vyenginevyo nisaidiwe suala hilo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Asha Mohamed Hilal: Ahsante sana Mhe. Spika, haidhuru wajumbe wanasema leo nimechafuka, naomba kuichangia ripoti hii. Kwanza nianze na samani yaani *furniture*. Kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti hizi samani

zilingane kutokana na ubora wake hapa tunavyozinunua ili ku-*save* fedha za serikali kwa sababu nilisema mfenesi haiwezekani kununuliwa kwa shilingi laki tatu. Kwa hivyo, tuweke viwango kutokana na ubora wa hii *furniture* maana nitakuwa siijui.
Pili, Baraza la Manispaa. Tayari tumeshapitisha sheria ya Mji Mkongwe na hapa palikuwa na mgogoro mkubwa baina ya Manispaa na Mji Mkongwe. Hawa wakurugenzi Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akae nao kitako ili kujua haki zao za msingi, yupi haki yake na yupi haki yake ili kuondoa migogoro na migongano iliyopo baina ya Mamlaka ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa.

Halafu nikija kwa Manispaa nije kwenye hawa ng'ombe. Siku zote hawa ng'ombe na punda tunawapigia kelele lakini naona bado. Tuweke mkakati maalum wa kuwadhibiti hawa kwa sababu wanaenea na wanatuchafulia mazingira ya mji.

Jengine ukurasa wa 133, nyaraka. Kwa kweli Mhe. Spika, nyaraka, vizazi pamoja na vifo vya huko Mambomsiige viko katika hali mbaya, yale mabuku ukiambiwa uyakamate basi utafanya hofu, utaona sijui yamekumbwa na matatizo gani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri yale mabuku kwanza tuyatafute mapya kwa kuanzia, tufanye *registration* tangu zile za mwanzo awamu kwa awamu ili kuwe na *datas* katika hali nzuri.

Vile vile hivi sasa ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia, kwa nini tusiingize kwenye kompyuta wale watu. Tungeanza kuwaingiza taratibu kwa mpangilio maalum, kuanzia mwaka gani mpaka mwaka gani tunajiwekea kiwango kwa muda wa miezi fulani tayari tumemaliza. Nafikiri tutatunza nyaraka zetu vizuri na zitaonekana vizuri kuliko hali iliyoko sasa hivi.

Mwisho Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya mwisho na mimi kutoa mchango wangu katika ripoti hii. Nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa kuwasilisha vizuri, halafu nipongeze wizara zote zinazohusika na ripoti hii kwa jitihada wanazofanya.

Mimi Mhe. Spika, nina *points* nne katika sehemu hii na nilikuwa naomba Mhe. Waziri anisaidie ufafanuzi. Kwanza, ukurasa wa 130 Afisi ya Mufti. Niipongeze kwanza ana afisi nzuri na ya kileo kabisa. Wenzetu wa kamati wameona matatizo madogo madogo kufunguliwa Afisi ya Maktaba na sehemu za kujisomea, hiyo si mbaya. Lakini mimi nataka nije juu ya suala la watoto yatima.

Hivi karibuni nilikwenda Afisini kwa Mufti na nikakutana na afisa anayehusika kuomba msaada wa watoto yatima ambao wameshafikia umri wa kusoma lakini wazee wao hawana uwezo huo. Akanambia kwamba wao kitengo hicho hawana lakini watanielekeza kuna *NGO's* zinasaidia. Kweli nilikwenda lakini nilipofika kule nilipokelewa vizuri isipokuwa wana masharti tu. Wanasema wao wanasaidia yatima kuanzia wa mwenzi mpaka miaka 10 na mtoto kukua ni umri wa mwezi mmoja mpaka miaka 18 huyo ndio anaweza akajitegemea. Sasa nikaona pana *gape* la miaka 10 mpaka 18 hii miaka minane atasaidia nani?

Ninaishauri wizara kwamba pamoja na kuwa sisi hatuhusiki sana na kusaidia yatima, lakini iko haja kwamba na wao wangefungua kitengo labda kuanzia hiyo miaka 10 kwenda 18 wakaweza kutoa msaada kwa watoto yatima. Kwa sababu wapo wengi na hivi sasa kuna matatizo mbali mbali watu wanafariki kwa maradhi yamekuwa mengi, ajali. Sasa naomba hili serikali walifanyie jitihada ili hawa yatima wapate haki zao za msingi.

Suala la pili nakuja kwenye suala zima la migogoro ya Misikiti. Kwa kweli muda mrefu kuna migogoro katika Misikiti na afisi imejitahidi kutatua lakini bado inaendelea. Kuna sehemu nyengine watu wanagombania Msikiti mpaka wengine wanajitenga wanageuza nyumba baada ya Msikiti uliokuwa umejengwa rasmi kwa dini. Sasa naomba na hili Waislamu mpaka tukafika hapo migogoro inakuwa mikubwa zaidi.

Ningelishauri bado Afisi ya Mufti ikafanya ziara mbali mbali katika Misikiti ili kuondosha mgogoro huu, kwa sababu Waislamu kugombana si jambo zuri. Hao wenzetu ndio wanaotambua misingi hiyo ya dini, sasa naomba na hili serikali ikalipa kipaumbele. Iko Misikiti mjini, mashamba nadhani wanaifahamu. Kwa hivyo, wachukue jitihada za kuweza kutatua.

Suala jengine nije ukurasa wa 132 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Nakumbuka hivi karibuni Bodi ya Wakfu ilipita kukagua mashamba ya wakfu pamoja na nyumba. Taarifa hiyo ilipatikana lakini namuuliza Mhe. Waziri, baada ya kupatikana mashamba ambayo wamekagua maeneo mengi hata Mfenesini, lakini watu sasa hivi wameyavamia. Je, yale maeneo ya wakfu yaliyovamiwa kama nyumba na mashamba, baada ya ripoti hiyo wizara imechukua hatua gani.

Jengine kuhusu vyeti vya kuzaliwa. Wamezungumza wenzangu waliozungumza lakini mimi nakuja upande mwengine. Hivi sasa kuna upotevu mwingi sana wa vyeti vya kuzaliwa, lakini faini inayowekwa kule kwenda kuchukua chengine ni kubwa kwa wanyonge, unatakiwa ukenda kule ulipe elfu arubaini upewe cheti kingine.

Sasa naomba na hili kwa wanyonge ni pesa nyingi tungepunguziwa ikawa elfu kumi na tano mpaka ishirini, angalau mtu umzindue kwamba ukipata kitu cha msingi uweze kukihifadhi ndio maana yake. Lakini tusiseme kuwa ile kama adabu na wengi wanashindwa. Sasa hivi watoto wakisoma jambo la kwanza ukitakiwa kazi upeleke cheti cha kuzaliwa. Sasa naomba na hili wizara itazame iweze kupunguza bei ili vijana wasikose kazi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nije kwenye changamoto. Imezungumziwa hapa kwamba sehemu ya Majaji bado hawajapatiwa vipando vya kwendea kwenye kazi na ni hatari. Kwa sababu jaji unaweza kwenda Mahakamani ukamfunga mtu miezi sita halafu kaka yake akakupakia kwenye gari akaipiga na mnazi ukafa ili kulipa kisasi cha ndugu yake. Sasa na haya madogo madogo yangezingatiwa ili kuwapa hali ya ulinzi majaji wetu na waweze kuipenda kazi yao.

Haiwezekani jaji unatoka mjini unapanda daladala mpaka Mfenesini, unahukumu halafu unangoja daladala unarudi, si utaratibu mzuri na tumeshawasemea sana katika Baraza hili. Kwa hivyo, naomba na hili kwa kumalizia basi majaji wetu wanaokuwa wanafanya kazi nje ya mji wasaidiwe vipando, kwanza kiwape moyo katika kazi, lakini pia kiweze kuwalinda katika hatari. Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru na mimi naunga mkono ripoti ya kamati.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, naomba kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe kupitia Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, kwanza nataka kwa mara nyengine tena nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa maelekezo yake na miongozo wanayoipa wizara yetu kila wanapotembelea katika shughuli zao za kamati katika wizara yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea kutoa ufafanuzi wa baadhi ya michango ya waheshimiwa katika ripoti yetu hii ya kamati naomba nianze suala zima alilolieleza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kuhusu makaazi ya Mhe. Waziri Kiongozi au Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika ripoti ya kamati imeeleza ni busara afisi yetu ikatafuta kiwanja katika maeneo mbali mbali na walitoa mfano kama Tunguu kwa ajili ya ujenzi wa Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi. Ukiangalia kwa sababu kutokana na wadhifa wake na eneo ambalo ilipo afisi yake kwa kweli sio pahala pazuri kiusalama, kweli eneo liko njiani sana na wakati mwengine

hata anapoingia afisini inabidi pale barabara kwanza ifungwe kwa ajili ya kumpisha Mhe. Waziri Kiongozi. Kwa hivyo, hili tunalichukulia kama ni changamoto katika afisi yetu, tunakuahidi Mhe. Mwenyekiti tutaweza kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti alieleza kilio chake. Kuna wakati fulani katika ziara yake ya kamati watendaji wangu wakuu pengine hata na mimi mwenyewe sikuwahi kushiriki katika kikao kile.

Mhe. Spika, kwanza tuombe radhi sana kwa hili ambalo limetokezea na tunaahidi halitotokezea tena. Lakini labda tu nijaribu kutoa ufafanuzi kwa yale ambayo yalikuwa yamejitokeza kwamba mimi kamati ilipokuja kwa bahati niliagizwa niende Kisumu Kenya kushiriki katika mkutano unaohusu *full security* na *climate change.*

Mhe. Spika, kutokana na hali ya mabadiliko ya hewa duniani sasa hivi na sisi zaidi wizara yetu inashughulikia na mambo ya maafa, kwa hiyo kuna masuala kama alivyosema Mhe. Juma Duni Haji hapa kwamba tunatakiwa tushiriki katika vikao hivi vya jumuiya kwa sababu kule sasa hivi ndio tunaanza *foundation* ya hii Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, lazima tuwe tunashiriki katika vikao ili kuweza kujua kile kinachopangwa, lakini sisi kama Tanzania kwa upande wetu Zanzibar tuweze kushiriki ili kuona kwamba katika yale yanayopangwa Zanzibar itafaidika kiasi gani ili tusije tukaachwa nyuma.

Suala la watendaji wetu kutokushiriki mheshimiwa atazidi kunisaidia lakini hata na hili na mimi naliomba sana kwamba watendaji wetu wasikwepe majukumu yao. Mhe. Spika, zinapokuja barua za vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, barua zinasambazwa katika maofisi yote lakini wakati mwengine utasikia watendaji wengine wanajitia sijui dharura hii, dharura hii, lakini muhimu kule tunajenga muungano mwengine.

Leo kama tunalalamikia muungano wetu wa Tanzania, sasa hivi tunaongeza tena muungano mwengine wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kama tunakuwa hatushiriki katika vikao vile kwa kweli itakuja kuwa ni athari kubwa kwa Zanzibar. Kwa sababu jambo likishapitishwa kule ina maana limekuwa *binded*, hatutosubiriwa tena kwamba Zanzibar walikuwa hawapo. Kwa hiyo, Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakuja kutoa ufafanuzi wa ziada lakini mimi katika kipindi hicho nilikuwa katika mkutano huo na Katibu wangu Mkuu alikuwepo Arusha.

Kwa sababu sasa hivi sisi Afisi ya Waziri Kiongozi tuna tatizo moja kwamba sasa hivi hatuna Katibu Mkuu, tuna Kaimu Katibu Mkuu. Kwa hiyo, sasa Naibu Katibu Mkuu ana-*act* kama ndio Katibu Mkuu. Mhe. Spika, kulikuwa kuna mkutano vile vile Arusha ambao ulikuwa unahusu masuala haya haya ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa mara nyengine nitamuagiza Katibu Mkuu wangu inapokuwa Kamati ya Baraza inakuja basi amuagize msaidizi wake, kwa sasa hivi atakuwa ni Mkurugenzi Mipango awe anashiriki kwa baadhi ya vikao ili Kamati ya Baraza inapokuja Katibu Mkuu aweze kutoa maelezo ya kutosha. Mhe. Spika, kama nilivyosema tunaomba radhi sana kwa hili na tunaahidi halitoweza kutokezea tena.

Mhe. Spika, katika ripoti ya kamati imeeleza ni namna gani ujenzi wa jengo letu la Afisi yaWaziri Kiongozi Pemba. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu hivi sasa jengo limeshamaliza kulikuwa kuna tatizo kamati ilipokuja Mwenyekiti alikuwa mkali. Lakini kama tulivyokuwa tunamuomba radhi fanicha tayari zimeshafika. Kwa sababu tulisema jengo letu lile haiwezekani kwamba jengo zuri jipya la kisasa tena tumejenga Pemba. Kwa mara ya mwanzo kwa ujenzi wa afisi Pemba basi Afisi ya Waziri Kiongozi ndio iliyoanza kufungua mlango. Kwa hiyo, tumejenga jengo jipya hatukuona haja sasa yale maviti mabovu yenye panya ambayo tulikuwa tunatumia katika afisi zetu zilizokuwepo sasa hivi tukahamishia katika jengo jipya.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa katika ripoti yake ndio maana alieleza kwamba Idara ya Mipango inatumia fedha nyingi sana. Pia akaeleza kwamba inatumia na vifungu vya idara nyengine. Mhe. Spika, ufafanuzi wa hili ni kwamba fedha zilizokusanywa katika idara nyengine ilikuwa ni fedha za ununuaji wa fanicha. Kwa sababu katika bajeti yetu katika kifungu cha fanicha tulikuwa hatuna pesa za kutosha kwa ajili ya fanicha za jengo lile la Afisi ya Waziri Kiongozi Pemba na tulitegemea jengo lile tulizindue katika Sherehe za Mapinduzi.

Sasa tukaona kwamba kwa kuwa jengo lile litakuwa linaingia taasisi zote, yaani idara zetu zote zitakuwa zinaingia katika jengo moja. Ndio maana tukahaulisha baadhi ya vifungu baada ya kushauriana na Katibu Mkuu kuja kunishauri mimi nikawakubalia wahaulishe vifungu. Lakini vifungu vyenyewe vilikuwa ni vifungu vile ambavyo vinahusu mambo madogo madogo kama hizo fanicha. Kwa hiyo, vifungu hivi ambavyo vilivyohaulishwa bado wataendelea kutumia wao wenyewe kwa sababu zile idara zao zitahamia katika hili jengo jipya.

Mhe. Spika, lakini pia muundo wa Idara ya Mipango kawaida shughuli zote inakuwa ziko chini ya Idara ya Mipango. Mhe. Spika, naona unaangalia saa nilikuwa najaribu kutoa ufafanuzi kwa sababu kama alivyosema Mwenyekiti alipokuja kwenye kamati Mtendaji Mkuu alikuwa hayupo lakini na mimi nilikuwa sipo hatukuweza kutoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, Idara ya Maafa kilio cha Mhe. Ali Denge Makame tumekisikia. Lakini Mhe. Spika, hili nadhani Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mwenyekiti wa

Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi akija na yeye atajaribu kutoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, maafa yale ya eneo la Kilimahewa tuliyaona na tuliagizwa twende tukaangalie hali halisi na mimi mwenyewe nilikwenda *physical* nikaona. Baadae ile bajeti kwa ajili ya kufidia wahanga wale ililetwa afisini na tukajaribu kuiangalia tukaipitia tukampelekea Mhe. Waziri Kiongozi na yeye akapitia akaifanyia marekebisho akampelekea Mhe. Rais tayari amekubali. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi alimpelekea barua Mhe. Waziri Kiongozi kwamba tayari imekubaliwa fedha zile milioni 27 zitolewe kwa ajili ya kuweza kununulia mabati pamoja na fedha taslim kwa wale ambao wamepata matatizo.

Sasa fedha hizi kwa ninavyojua Waziri wa Nchi (AR) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi ameshamuagiza Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kutoa fedha hizi. Lakini mpaka sasa hivi inaonesha labda pengine kutokana na hali ya umeme pale kidogo mapato yalikuwa yana ukwasi ukwasi, nafikiri sasa hivi Mhe. Waziri atakuja kutoa ufafanuzi hali ikoje. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Ali Denge Makame awaambie wananchi watulie ile fidia yao wataweza kupatiwa.

Mhe. Spika, pia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliwahi kuuliza kuna watu wanapigwa na mnazi, kuna watu wanaangukiwa na mambo mbali mbali. Alieleza vigezo gani vinavyochukuliwa katika suala zima la maafa.

Mhe. Spika, suala la maafa kwanza linataka taaluma kubwa. Labda kuna siku moja nitakuja kumuomba Mkurugenzi wangu wa Idara ya Maafa tuje tufanye semina maalum kuelezea ni namna gani ya maafa yanapotokezea. Kwa sababu kweli tunapata matatizo mengi kwa wananchi. Suala la maafa sio kama serikali inalipa fidia kwa yule mtu ambaye amepata maafa, hili ndio nilikuwa nataka niliweke wazi.

Mhe. Spika, Idara ya Maafa tunatakiwa tuwe na mfuko wa maafa. Katika sheria umo lakini kwa bahati mbaya sera tulikuwa hatuna. Sasa hivi tumo katika kukamilisha sera ya Idara ya Maafa ambayo itaelezea nini mamlaka ya Idara ya Maafa na taasisi nyengine majukumu yao vile vile. Kwa hiyo, hata ule mfuko wa maafa ukishaanzishwa jukumu la serikali linakuwa kwanza yanapotokezea maafa.

Mhe. Spika, kwanza kuna tafsiri ya maafa inayosema kwamba maafa ni janga linalokuwa kubwa linatokezea wananchi kwa kawaida hawawezi kulimudu.

Kwa hiyo, inapotokezea *gharka* mfano kama kimbunga tunatakiwa sisi kwanza tutoe *shelters* kwa wale ambao wamepata maafa, tuweze kuwapatia sehemu ya *camp*, tuweze kuwapatia chakula, madawa na mambo mengine ambayo wasiweze kuathirika. Lakini sio kujenga nyumba iliyoanguka au iliyoungua moto. Mhe. Spika, haya mambo yanataka ufafanuzi mkubwa sana.

Mhe. Spika, tunasikia watu wanagongwa na magari, nyumba zinaungua na kadhalika. Kwa utamaduni wa wenzetu nyumba inapoungua inatakiwa nyumba ziwekewe bima lakini huku kwetu hatuna. Ndio maana tutakapoleta ile sera ya maafa ndio itaelezea hasa ni namna gani maafa yanavyotokezea, nani atakayeathirika, nani atawajibika na suala la maafa lina mikono mingi.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, nikitaka kutoa ufafanuzi wa suala zima la maafa naweza nikachukua labda muda wa dakika 45. Kama nilivyoahidi hili tutajaribu kuandaa utaratibu itakapokuja ile sera ya maafa tutafanya semina atleast ionekane ni namna gani serikali inavyoshughulikia masuala ya maafa.

Mhe. Spika, jengo la Baraza la Wawakilishi tunategemea mwishoni mwa mwezi huu mjenzi aliahidi kwamba atatukabidhi, kwa hiyo tunategemea kikao cha bajeti tunaweza kwenda kutumia jengo letu jipya la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, jengo la Pemba limeelezwa lakini zaidi tumeombewa sana na Mwenyekiti wa Kamati kwamba tuanze kuingiziwa fedha ili tuweze kukamilisha ujenzi wetu wa kule Pemba. Kwa sababu kidogo hauridhishi, suala la magari Mhe. Waziri wa Fedha ameshalitolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, kutokana na muda wako nadhani mengine yaliyobakia tutakuja kuyazungumza katika kikao cha bajeti kinachokuja. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kukushukuru, ahsante.

Mhe. Spika: Niongezee jambo dogo sana kabla sijamwita Waziri mwengine anayefuatia. Jengo la Baraza la Wawakilishi kuna shughuli tatu kubwa. Shughuli za ndani ya Ukumbi ambazo mjenzi ameahidi atazimaliza mpaka kufikia wakati unaohusika. Shughuli za nje kumaliza *marble* hizo zinasua sua kidogo kutokana na hali ya mvua. Lakini ndani ameahidi atawahi wakati.

Lakini kuna matatizo mawili makubwa sana ambayo inabidi yafanyike ili kuwahi muda. Moja ujenzi wa barabara na *parking*, kazi hiyo itafanywa na serikali, UUB watatwambia nini pengine wanaweza wakatueleza. Kazi nyengine ambayo ni kubwa sana ni habari ya *transformer* nayo iko katika mikono yetu ya serikali. Hatua zimechukuliwa zimechelewa sana kwa kweli kufuatana na taratibu za kisheria, sheria za manunuzi, mambo ya tenda na kila

kitu. Lakini kimsingi hatua ya mkandarasi kupewa fedha naona nayo imekamilika zile ambazo zimetakiwa na taratibu za sheria.

Sasa muda ulikuwa ni mfupi tutaona kama anaweza kuwahi kuleta kwenye karibu ya mwisho wa mwezi huu. Sasa shughuli hizo zilizobaki mbili kubwa ambazo zimo katika mikono ya serikali zinaweza zikakwamisha shughuli hiyo, lakini na mjenzi nae shughuli yake moja ya nje inaweza isizuie, lakini za ndani ni muhimu azimalize pamoja na ku-*test central air-condition* ambayo inategemea *transformer* iliyoko upande wetu. Basi nilitaka niongeze hayo tu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kulikuwa na hoja tatu tu ambazo naomba nizitolee ufafanuzi. Moja Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu alionesha *concern* yake kwamba baadhi ya Makatibu Wakuu hawahudhurii katika wito au vikao vya kamati na alisema baadhi tu. Mimi *observation* hiyo siipingi kwa sababu yeye ndio yuko kwenye kamati, sasa anachosema tu kwamba tutajitahidi kuhakikisha kwa kushirikiana na Afisi ya Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi kuona kwamba Makatibu Wakuu au Manaibu wao wanahudhuria katika kamati kama sheria au maelekezo ya serikali yanavyosema.

Isipokuwa naomba tu wale Makatibu wa Kamati wajitahidi sana kupanga pamoja na Makatibu Wakuu kwa sababu najua Makatibu Wakuu nao wana *schedule* yao, sasa naomba sana wapange wakubaliane ile tarehe. Lakini kwamba wakache vikao nafikiri hiyo sio utaratibu mzuri na wala sio lengo lao. Kwa hiyo, hili tutalichukua kuhakikisha kwamba Afisi ya Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi inazungumza nao vizuri tuone kwamba mafanikio yetu kati ya Serikali na Baraza yanakwenda ipasavyo.

Mhe. Spika, suala la pili Mhe. Juma Duni Haji alionesha nae *concern* kubwa juu ya Wawakilishi wetu wa Zanzibar katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, namshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma ametolea ufafanuzi. Lakini nataka kumwambia tu Mhe. Duni kwamba tuna idara maalum, idara hii ni maalum kwa sababu ina Katibu Mkuu kamili inaitwa Idara ya Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa, tunayo iko chini ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wao ndio dhamana wa kuratibu vikao vyote vile na kuhakikisha mpaka fedha za safari zile za vikao vya wataalam wametiliwa kwenye bajeti yao. Kwa hiyo, wao mtaalam ikifika kwenda kikao gani basi *process* inaandaliwa *funding* inafanywa na afisi yake hii.

Sasa najua mtiririko uliopo kuna vile vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwanza kuna vikao vya wataalam, vinafuatiwa na vikao vya Makatibu Wakuu, Mawaziri, halafu mwisho wenyewe *summit* Marais. Sasa Marais si mara

nyingi, lakini mara nyingi tunaishia Mawaziri. Kwa hiyo, wataalam wakenda wanakutana kule na Makatibu Wakuu wao, wanawa-*brief* Makatibu Wakuu, Makatibu Wakuu wanakuja wanawa-*brief* Mawaziri na vile vikao vya mwisho mara nyingi tunakuwa pamoja.

Kwa hiyo, kunakuwa na *very close linked* na *relationship* pale inatendeka. Hutokea bahati mbaya tena hilo tumeona *observation* hii kwamba vile vikao wale mara nyingi zile ratiba hawazifuati, wataleta barua kikao fulani, mwisho wanaleta dakika za mwisho kwamba kikao tumekivunja. Mimi imeshawahi kunitokezea mwenyewe mara mbili tatu nimeshakwenda mpaka kwenye venue ya mkutano naona tangazo pale "Tunasikitika kikao kimeahirishwa mpaka baada ya siku mbili".

Mhe. Spika, tunamsifu sana Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mhe. Kamala hodari sana, anawasiliana na sisi anatuandikia barua mawaziri sote tuliokuwepo, anatualika vikao vile na kwanza wataalam wao kule, Katibu Mkuu wa Afisi ya Jumuiya nae anatushirikisha. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Spika na Baraza lako tukufu kwamba kwa kweli tunashirikishwa ipasavyo na tunashiriki ipasavyo.

Mhe. Spika, nashukuru Baraza hili mara nyingi sana walikuwa wanatuelekeza wanatwambia hapa labda walikuwa na matatizo ya fedha sasa hayapo tena, yanasimamiwa vizuri, yanaratibiwa vizuri kabisa na *interest* Zanzibar zinalindwa na kuna mifano mingi tu. Zaidi kuna wataalam wetu wamefika hadi kutiwa katika Sekretarieti za Jumuiya ya Afrika Mashariki na wanalipwa na Jumuiya hiyo kwa baadhi ya vikao. Hii inaonesha *competency* yao wanayo na kujiamini kwao na kuitambua Zanzibar. Mhe. Spika, naomba kumhakikishia Mhe. Juma Duni Haji kwamba hili *is well take and care.*

Mhe. Spika, la mwisho ni suala la Mhe. Ali Denge Makame (Profesa) nafikiri Mhe. Hamza Hassan Juma kalizungumza vizuri, mimi nimalizie tu kwamba maandalizi yote ya malipo yale yamekamilika, wamechelewa kidogo kwa sababu ya kufanya uhakiki wa wale wanaodai. Unajua mambo haya kidogo iki-*involve* watu na mapesa yana matatizo yake. Kwa hiyo, watu wenyewe wahasibu wa mapesa mapesa wale wakasema aaa hebu tuka-*verify* tuwajue hasa anayehitajia bati yupi, anayehitajia nini yupi, baada ya *verification* hiyo nafikiri sasa tuko tayari Wizara ya Fedha tutashirikiana na Afisi ya Waziri Kiongozi na mwenyewe Mhe. Mwakilishi twende tukalipe kabla ya maafa mengine, Mwenyezi Mungu atustiri.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, nimepata masuala mawili matatu na ni vizuri niyatolee ufafanuzi. La kwanza ni hili tatizo la madaktari kutokwenda kutoa ushahidi. Mhe. Spika, ni juzi tu hapa

tumepitisha sheria kuhusu hii Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kisheria kabisa tukaweka kamati maalum ya kusukuma usikilizaji wa kesi ambao daktari tumemuingiza katika kamati ile kwa kupambana na tatizo ambalo tumekuwa nalo katika Mahakama wakati tunapokwenda.

Mhe. Spika, jengine ni migogoro ya Misikiti. Hili Afisi ya Mufti mara nyingi inakuwa inapanga ratiba na inapita katika misikiti mbali mbali kuwaelimisha watu juu ya suala hili. Kwa wito wa Mhe. Ali Abdalla Ali tutaendelea nayo kazi hiyo, maana tunayo na inafanywa na wakati mwengine Mufti mwenyewe huwa anashiriki kupita katika misikiti kuwafahamisha masuala haya.

Suala jengine ni maeneo ya mashamba ya wakfu yaliyovamiwa. Ni kweli ile bodi imemaliza kazi ya kutembelea mashamba haya na imegundua, imeiagiza Kamisheni ya Wakfu kuchukua hatua mbali mbali juu ya masuala haya.

Hatua ya kwanza ambayo Kamisheni ya Wakfu inakusudia kuifanya ni kuwaita wale wavamizi. Mhe. Spika, ukijenga nyumba juu ya shamba ya wakfu umeshadhulumu na dhulma ile inaendelea, maana wafaidika wa wakfu ule unakuwa umeshawafungia, kama ni msikiti au kama shughuli yoyote inakuwa hakiendi umechukua wewe na umejenga nyumba pahala pale.

Jambo la kwanza unatakiwa ufahamu madhara yake kwa sababu ni haki ya binadamu ile na *haqil adamiya* haisameheki, utakwenda kukumbana nayo hata kama utafanya ibada kiasi gani hapa lakini mwenyewe *Ghafur Rahim*. Hiyo inatakiwa kila mtu aliyejenga nyumba katika shamba la wakfu alielewe kwamba yupo juu ya shamba la wakfu. Ni vizuri awaambie na wanawe hasa, wanangu tumejenga nyumba juu ya shamba ya wakfu hii kwa hivyo wachukue hatua ya kuchukua. Ni hatari sana mbele ya safari.

Mhe. Spika, baada ya kwisha kuwaita na kuwaelimisha juu ya suala hilo waliovamia lakini hatua itakayofuatia hapo sasa kwa sababu bado Kamisheni ya Wakfu itakuwa ina dhima, ni kuwafikisha watu hao kwenye vyombo vya sheria. Lakini kwa nini tungojee hivyo, ni vizuri mwenyewe akajua. Kwa sababu haiwi serikali ambayo katika yale mashamba inayoyachukua inaendelea kulipa fidia kila siku kwa wahusika na wafaidika ya nyakfu zile mbali mbali. Hii ni haki ya binadamu ni vizuri sote tujue kwamba haisameheki mpaka irekebishwe inapofaa kurekebishwa.

Mhe. Spika, vyeti vya kuzaliwa kama alivyojibu Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi tulipokuwa tukijadili masuala mbali mbali hapa tungojee Waziri wa Fedha atupunguzie mgao au makusanyo kutoka Afisi ya Mrajis ili tuweze kupunguza hivi vyeti. Kwa sababu sasa hivi anatudai huyu shilingi milioni 258 lazima tumpe na hizo ndio zinazotumika kwenye mishahara na

mambo mengineyo. Kwa hivyo, itabidi bajeti ijayo hili lirekebishwe ili tuweze kupunguza hivi vyeti. Ni suala la kuzungumzwa pamoja katika serikali.

Suala la vipando vya Majaji, hili nalichukua na tunajaribu kuhamasisha kwamba watafute usafiri lakini pia tunataka tuweke usafiri wa pamoja. Lakini jaji ni mtu huru, unaweza ukawepo usafiri wa pamoja ukasema kwamba utawakusanya wote saa mbili, pengine saa mbili hawajawa tayari, sasa itabidi uanze kumngojea jaji wa kwanza atoke pale saa tatu, jaji mwengine pengine anaondoka pale saa nne, au jaji mwengine ulete na habari katika kituo lakini ameshapeleka taarifa kwamba hiyo kesi leo huko sitoisikiliza naahirisha mpaka tarehe kadhaa, wale makarani ndio wanatoa taarifa hizi, ni ngumu kidogo. Ni vizuri hasa wakawa na usafiri wao wenyewe ndio inakuwa nzuri. Mhe. Spika, unalifahamu suala hili maana hiyo kazi ulifanya. Baada ya hayo sina zaidi nashukuru sana.

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa kutuusia kama ulivyoiusia nafsi yako juu ya hatari ya mali za wakfu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, nina sehemu nne ambazo naomba nizitolee ufafanuzi. Kwanza ni suala la mitaro ya maji machafu au maji ya mvua yanayotoka Kwahani, yanayoangukia Kwaalinatu, yanayokwenda zake Bomani mpaka Maisara baharini.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) asiwe na wasi wasi watampitisha tu katika Jimbo la Kwahani, tena tuko pamoja jirani pale nitamsaidia. Kwa hivyo, mitaro maji mpaka sasa hivi yanakwenda vizuri mvua zinakwenda, maji yanajaa lakini yanapita. Hilo mpaka sasa hivi liko vizuri asiwe na wasi wasi.

Mhe. Spika, jengine ni shamba la mboga mboga. Ukweli wenzetu tunaoshirikiana nao nchi ya Misri wameweza kukamilisha vile vifaa vyote ambavyo vilikuwa vinahitajika kuhusu mradi huo na bahati nzuri na sisi sehemu kubwa tumeshaikamilisha. Suala lililobakia ni kwenye ujenzi wa shimo ambalo ni kubwa sana, watendaji wetu wanalichimba kidogo kidogo lakini linaonekana linaelekea pahala pazuri sana. Hata hivyo, wamejaribu kufanya majaribio ya mboga mboga vipi zitaota mbegu mbali mbali, nafikiri mboga hizo kwa bahati nzuri zimefika mpaka hapa Baraza la Wawakilishi na baadhi ya waheshimiwa wameshazionja mboga hizo. Ni mboga nzuri tamu na hazina matatizo yoyote.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kuhusu suala la Mji Mkongwe. Mhe. Spika, mvutano wa Baraza la Manispaa na Mji Mkongwe uko chini ya Wizara na

unafanyiwa kazi katika ngazi ya utendaji yenye kupitia sheria zinazoingiliana ili zifanyiwe ufafanuzi kuondosha mgongano huo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuhusu *by laws* zimetayarishwa na sasa hivi ziko katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu zinafanyiwa utaalam zaidi.

Mhe. Asha Moh'd Hilal uzururaji wa wanyama hatua zinachukuliwa na kukamilisha by laws kutaleta msukumo mzuri na yule ambaye anamuachia ng'ombe au mbuzi wake kuzurura ovyo hatua za kufaa zitachukuliwa.

Suala jengine ni kuhusu habari kati ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa, hizi kila mtu ana sheria yake. Lakini hata hivyo, ziko katika utendaji wa mwisho mwisho wa kuwa inazifanyia ngazi ya utendaji ili kupatiwa sheria zinazoingiliana zifanyiwe marekebisho. Sheria nyengine ni zile za Halmashauri na Baraza la Manispaa zipatiwe kwa kuwashirikisha taasisi hizi mbili.

Mhe. Haji Omar Kheir: (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nipate kuwashukuru wachangiaji 12 ambao wameuliza maswali na kutaka ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo tumeyaainisha kwenye ripoti yetu. Niwashukuru wale wote ambao wamefanya kazi hiyo. Ni imani yangu kwamba kama muda ungekuwepo basi wangekuwepo wachangiaji zaidi ya hawa ambao wamejitokeza.

Wachangiaji ambao wamechangia ni:

1. Mhe. Ali Denge Makeme
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Zahra Ali Hamad
5. Mhe. Ramashan Nyonje Pandu
6. Mhe. Juma Duni Haji
7. Mhe. Asha Moh'd Hilal
8. Mhe. Ali Abdalla Ali
9. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi
10. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
11. Mhe Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora
12. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ

Kwa jumla nawashukuru sana kwa michango yao ni imani yangu kwamba nia na madhumuni ya utaratibu wa kuwasilisha ripoti za kamati katika kipindi hiki cha mwezi wa Aprili, ni kwamba yale yaliyoelezwa kwenye ripoti za kamati za

kudumu za Baraza la Wawakilishi yatarekebishwa tutakapokuja kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, niruhusu niseme moja tu ambalo Dk Mwinyihaji Makame amelitolea ufafanuzi na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu alilizungumza sana tena kwa uchungu sana, juu ya suala la watendaji.

Mhe. Nyonje amenukuu kifungu cha sheria. Nakumbuka Baraza la mwaka 2000/2005 nilitaka kuwakamata kwa mujibu wa uwezo wa kamati makatibu wawili wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wakati ule na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa uwezo wa sheria na kanuni zetu, tunao uwezo wa kumkamata mtendaji yeyote ambaye atashindwa kushiriki kwenye Kamati za Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, pamoja na maelezo mazuri, naomba hili nilisisitize sana aliyoyatoa Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Spika, uungwana mkubwa unafanywa na Afisi ya Baraza la Wawakilishi wa kuwaarifu watendaji wakuu wa serikali, kushiriki kwenye kuthibitisha ratiba za kamati wakati kamati zinataka kufanya shughuli zake. Ninachotaka kusema ni kwamba baadhi ya watendaji wakuu huwa hawashiriki hata kwenye kile kikao cha kuthibitisha ratiba. Sasa hapa ndipo panapoanza tatizo kwa sababu kwenye mjadala wa kuthibitisha ratiba mna *option* ya kubadilishana siku ambazo umepangiwa na makatibu wakuu wenzio. Sasa unapokuwa hufiki siku ile, halafu baadae ukawa hutoi sababu za msingi basi inaonesha hii ni dharau.

Mhe. Spika, kwenye vikao vyengine nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, nilishawarejesha maafisa wa ngazi za chini, yaani maafisa wadogo wadogo kwa sababu hawana mamlaka ya kuweza kujibu hoja za kamati. Nadhani sasa hivi tujenge utamaduni, pamoja na kwamba kamati zinakutana na watendaji, lakini kwa uzoefu wa mabunge mengine, kama Bunge la Jamhuri ya Muungano basi mawaziri wanashiriki kwenye shughuli za kamati.

Mhe. Spika, nadhani kama sijakosea tuliwahi kupitisha huu utaratibu, kuwa mawaziri ni sehemu ya wajumbe wa kamati na haki zote wanastahiki kupewa. Kwa hivyo, nadhani kwa sababu watu wetu sisi hasa ni mawaziri, basi Mhe. Spika, naomba serikali izingatie suala la mawaziri kushiriki kwenye shughuli za kamati. Pia makatibu wakuu wawemo, lakini kama katibu kenda Geneva au kenda New York basi utatujibu wewe waziri, badala ya kuwa tunabakia hewani tu. Kunakuwepo na mambo muhimu na ya msingi ambayo yanahitaji ufafanuzi lakini hayapati ufafanuzi.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba ni vizuri uungwana huu wa Baraza la Wawakilishi wa kuahirisha makatibu wakuu kuja kuthibitisha ratiba za

kutembelea wizara yao. Mhe. Spika, sidhani kama kungekuwa na mtu ambaye angeweza kutoa kisingizio kwa sababu kama Katibu Mkuu ana safari ya lazima kwenda Geveva kwa maslahi ya nchi, sidhani kama kamati itamzuia. Lakini tutapata maelezo ambayo na sisi tutayaeleza kwenye kamati kwa nini Katibu Mkuu yule hakushiriki kwenye mjadala wa kamati.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo naomba niwashukuru wote waliochangia na wale ambao pengine walikuwa na hamu ya kuchangia ripoti yangu, lakini kwa sababu ya muda hawakupata nafasi hiyo. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji, wale wanaoikubali na kuipokea ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ripoti iko tayari kufanyiwa kazi na serikali, taarifa ya utekelezaji wa ripoti hii na nyenginezo ziletwe katika Afisi yetu ya Baraza.

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kwa mkutano huu wa kumi na tisa, sasa zimekamilika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamuomba Mhe. Waziri Kiongozi atoe hotuba ya kufunga mkutano huu, naomba na mimi nichukuwe nafasi ya kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na mawaziri, kwa mashirikiano makubwa mliyotupa katika kuendesha shughuli za mkutano huu wa kumi na tisa.

Mkutano huu kidogo ulikabiliwa na shughuli nyingi na muda ulikuwa mchache, lakini mmevumilia na tukaweza kufanyakazi mpaka kuzimaliza shughuli zote leo siku ya Jumamosi ya tarehe 03/04/2010, nawashukuru sana tena sana.

Nichukuw nafasi hii pia kuwashukuru watendaji wakiongozwa na Katibu, wote nao nafikiri wametoa huduma vizuri sana kwa Waheshimiwa Wajumbe ili shughuli zetu hizi ziende kwa ufanisi. Niwashukuru watendaji wa wizara mbali mbali ambao wamekuwa wanahudhuria na kufuatilia kwa karibu shughuli

ambazo zilikuwa zinawahusu, kiasi cha kwamba walikuwa wanawasaidia Waheshimiwa Mawaziri ili kuweza kujibu hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe.

Vile vile nisiache kuwashukuru waandishi wa habari ndugu zetu wa Sauti ya Tanzania Zanzibar, ndugu zetu wa Televisheni Zanzibar na waandishi wengine wa habari ambao watasaidia kuchukua taarifa za mkutano wote huu wa Kumi na Tisa na kuzitoa kwa wananchi kwa njia ya televisheni, redio na magazeti. Nawashukuru sana kwa mashirikiano yenu pamoja na Afisi yetu hii ya Baraza la Wawakilishi.

Nawashukuru pia wageni wamekuwa wakija hapa na kusikiliza majadiliano yetu haya kwa faida ya wananchi wote. Sasa kwa kuwa muda uliobaki ni mdogo na hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi itachukua zaidi ya muda uliopo hivi sasa kufikia saa 7:00. Kwa hivyo, nimuomba basi Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kutoa hoja ili kuongeza muda mpaka pale Mhe. Waziri Kiongozi atakapomaliza hotuba yake tuweze kufanya shughuli hii. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi karibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba kwa kuwa shughuli zetu bado hatujamaliza, tunategemea Mhe. Waziri Kiongozi atasoma hotuba yake pengine itazidi muda wetu wa kawaida. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liongeze muda mpaka hapo Mhe. Waziri Kiongozi atakapomaliza hotuba yake. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Kwa furaha kabisa sasa namuomba Mhe. Waziri Kiongozi, mara baada ya adhana.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KUAHIRISHWA BARAZA

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendesha shughuli za Baraza lako tukufu kwa ufanisi. Pili, nakushukuru wewe Mhe. Spika kwa kuuongoza mkutano huu kwa

hekima na busara kubwa hasa tulipokuwa tunajadili suala zito na muhimu sana kwa mustakabali wa taifa kuhusu mswada wa sheria ya kura ya maoni.

Tatu, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwa kuuliza maswali mazuri kuhusu utendaji wa shughuli za serikali na kujadili hoja mbali mbali zilizowasilishwa katika Baraza lako tukufu.
Mwisho, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri maswali yote yaliyoulizwa na kutoa ufafanuzi wa hoja.

Mhe. Spika, katika mkutano huu Waheshimiwa Wawakilishi waliuliza jumla ya maswali 66 ya msingi. Vile vile mkutano huu ulijadili miswada mitano ya sheria na kupokea ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza lako tukufu. Miswada na ripoti hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Mswada wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika kesi za madai na utaratibu wa mwenendo wa madai dhidi ya Serikali.
2. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Michezo na kuanzisha Sheria Mpya ya Baraza la Taifa la Michezo.
3. Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na kuanzisha Sheria Mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.
4. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Uvuvi na kuweka masharti bora yanayohusiana na usimamizi na maendeleo ya uvuvi Zanzibar.
5. Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni.
6. Ripoti za Kamati 5 za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mswada wa kwanza kujadiliwa na Baraza lako tukufu ulikuwa mswada wa sheria ya kuweka haki na wajibu wa serikali katika kesi za madai na utaratibu wa mwenendo wa madai dhidi ya serikali. Madhumuni ya mswada huu ni kulinda na kuzuia mali za serikali zisikamatwe wakati serikali inapokabiliwa na kesi za madai mahakamani. Pamoja na kwamba sheria hii inazuia utoaji wa amri ya kuuza mali za serikali inapokabiliwa na kesi za madai, Serikali itaendelea kuwa na wajibu wa moja kwa moja wa kulipa madeni inayodaiwa na watu mbali mbali kama ilivyo kwa watu binafsi.

Kwa kuwa uwajibikaji ni moja ya misingi madhubuti ya utawala bora, maafisa wa serikali wanatakiwa wawe makini zaidi katika kutekeleza wajibu wao, ili kuiepusha serikali kushitakiwa kwa kesi za madai. Ili kudhibiti vitendo vya

uzembe afisa wa serikali atakayeisababishia serikali hasara kwa kushindwa kutoa ushirikiano katika kesi za madai, atalazimika kulipia fidia hasara hiyo. Hatua hii bila shaka itaidaidia sana serikali kuwadhibiti maafisa wa serikali wanaokwepa kutekeleza wajibu wao kwa kuamini kuwa serikali haistahiki kushtakiwa mahakamani.

Mhe. Spika, mswada wa Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo unalipa Baraza la Michezo uwezo wa kusimamia maendeleo ya shughuli za michezo hapa Zanzibar. Ili nchi yetu iweze kuendeleza michezo na kutupatia wanamichezo walio bora wa kutuwakilisha katika mashindano mbali mbali, ya ndani na ya kimataifa. Baraza la Michezo linapaswa kuvisaidia vyama vya michezo kutafuta makocha wazuri, kutafuta vifaa na viwanja vilivyo bora. Kuna haja ya kuandaa programu maalum za mafunzo ya ukocha wa michezo.

Mhe. Spika, ninakumbuka Chuo cha Ualimu Nkurumah kilikuwa kikiandaa diploma ya michezo katika miaka ya 90 kama sikosei. Kwa bahati mbaya kozi hiyo sasa imefutwa. Nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kuwa ipo haja ya kufikiria sana kurudisha mafunzo ya namna hii au yanayofanana na haya maskulini, ili vijana wetu wapate walimu bora wa michezo. Hapana shaka mafunzo haya yaliwasaidia sana walimu wakati ule kuibua na kukuza vipaji vya michezo maskulini. Kama kuna mahali pazuri pa kukuza na kuinua vipaji vya michezo kwa watoto basi ni skuli. Kama Waswahili wasemavyo, “Udongo upate ulimaji”.

Mhe. Spika, hivi sasa tunashuhudia mtindo wa baadhi ya wananchi wa kujenga nyumba na vituo vya mafuta katika viwanja vya michezo. Jambo hili linazorotesha sana juhudi na maendeleo ya shughuli za michezo, kwa sababu tukifanya hivyo tunawanyima watoto wetu sehemu za kuchezea. Kwa kiasi kikubwa ukosefu wa viwanja vya michezo unadumaza vipaji vya wanamichezo. Nimebaini kuwa baadhi ya skuli hazina viwanja vya michezo. Mwezi uliopita nilikuwa katika ziara ya kutembelea baadhi ya skuli, hasa skuli ya Ngwachani katika jimbo la Mhe. Abass Juma Muhunzi. Nilishituka sana kuambiwa kuwa skuli haina kiwanja cha michezo. Hapana shaka hali hii inadumaza maendeleo ya kielimu na michezo kwa jumla.

Mhe. Spika, mtakubaliana nami kuwa Sekta ya Michezo inakabiliwa na matatizo kadhaa yanayochangia kurejesha nyuma maendeleo ya michezo. Kama nilivyokwishaeleza hapo awali makocha, vifaa na viwanja vya michezo vina umuhimu mkubwa sana katika kuendeleza michezo. Nilipokuwa katika ziara hiyo ya Skuli ya Ngwachani, niliwashauri walimu watafute kiwanja katika maeneo ya karibu, kiwanja ambacho kinaweza kikafanyiwa matengenezo. Kwa bahati nzuri katika maeneo ya jirani kulikuwa kuna kiwanja ambacho hali yake sio nzuri sana, na tulikubaliana kwamba tushirikiane basi serikali, walimu na

wazee katika eneo lile, ili kuhakikisha kwamba vijana wetu basi wanapata kiwanja kwa ajili ya kufanya shughuli mbali mbali za michezo.

Mafunzo ya makocha yanahitaji kupewa uzito unaostahiki kwani pamoja na kwamba makocha wetu wengi ni wazuri, lakini wanahitaji mafunzo ya mara kwa mara ili kukuza ujuzi na mbinu za kufundishia. Vyama vya michezo vinapaswa kuandaa semina na mafunzo ya makocha wa michezo ili kuondoa upungufu wa makocha uliopo.

Mhe. Spika, suala la mafunzo ya makocha linatakiwa liende sambamba na kuanzishwa kwa vyuo vya Michezo (*Sports Academies*). Vyuo vya michezo vinaweza kusomesha wanamichezo kwa ajili ya nchi za Afrika Mashariki na Kati ili kutuingizia fedha. Natambua kuwa utekelezaji wa jambo hili ni mgumu, hasa tukizingatia kuwa vyama vya michezo vinakabiliwa na upungufu wa fedha. Kuna haja basi ya kuanzisha miradi ya uchumi ili vyama vyetu vya michezo viweze kujitegemea.

Mhe. Spika, tunaweza pia kuimarisha michezo kwa kuanzisha michezo mipya kama vile michezo ya baharini, Marathon ya kimataifa iliokuwa ikifanyika siku za nyuma hapa Zanzibar. Michezo hii itasaidia sana kuvutia idadi kubwa ya watalii. Halikadhalika, Baraza la Michezo linaweza kufufua michezo na kuendeleza michezo kama *Cricket, Golf, Table Tennis* na Judo. Michezo ya namna hii inaweza kuiletea sifa kubwa sana nchi yetu.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu pia lilijadili mswada wa sheria ya kufuta sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na kuanzisha sheria mpya ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Mswada huu una lengo la kuipa Mamlaka ya Mji Mkongwe uwezo wa kusimamia hifadhi ya Mji Mkongwe ili uwe wa haiba ya kuvutia. Mamlaka ya Mji Mkongwe inao wajibu mkubwa wa kudhibiti vitendo vinavyoharibu mandhari ya mji huo. Hivi sasa tunawashuhudia madereva wanaoingiza gari zenye uzito mkubwa katika Mji Mkongwe, licha ya kuwepo sheria inayokataza jambo hilo. Mbali na udhibiti wa magari makubwa katika Mji Mkongwe, Mamlaka hiyo kwa kushirikiana na idara ya utoaji wa leseni za magari, zinaweza kubuni mbinu na njia za kupunguza msongamano wa magari katika maeneo mbali mbali ya Mji Mkongwe. Vile vile kuna haja ya kuwataka wamiliki wa nyumba za Mji Mkongwe kuzipaka rangi nyumba zao, kuondoa vifusi na magugu karibu na nyumba hizo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mji Mkongwe hivi sasa una upungufu mkubwa wa maeneo ya kupumzikia watu, naiomba mamlaka hiyo ibuni na kutafuta maeneo mapya kwa ajili ya kupumzikia watu. Bustani ya Forodhani pekee haiwezi kukidhi matumizi kwa wananchi wote wa Mji Mkongwe. Kwa hivyo, kuna haja

ya kuanzisha bustani mpya na kuziendeleza zile zilizopo kama bustani ya "*Jamhuri Garden*". Mji Mkongwe ni hazina kubwa katika kukuza biashara ya utalii. Ili kufikia lengo hili wananchi wa Mji Mkongwe wanapaswa kuelimishwa jinsi ya kudumisha usafi wa huo. Vile vile wafanyakazi wa sekta za biashara na utalii wahimizwe umuhimu wa kutoa huduma zilizo bora, ili kuwavutia wageni wengi zaidi. Ninaamini juhudi hizi zikiimarishwa, basi biashara na utalii kwa ujumla utaimarika sana.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe una fursa nzuri ya kukuza uchumi iwapo tutaimarisha vivutio vya utalii kama vile fukwe, migahawa na boti za kutembeza watalii. Vile vile kuna haja ya kuanzisha huduma za hoteli katika majahazi pembezoni mwa pwani ya Mji Mkongwe sambamba na michezo ya baharini. Ili kuongeza idadi ya vivutio vya utalii Zanzibar, natoa wito kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe washirikiane na washirika wa sekta ya utalii na utamaduni kuimarisha Tamasha la Filamu za Nchi za Jahazi, Sauti za Busara na Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari ili waweze kuutangaza Mji Mkongwe. Matamasha ya namna hii yatawasaidia sana wafanyabiashara kuongeza mapato.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu limepata pia fursa ya kupitisha mswada wa sheria mpya ya uvuvi. Madhumuni ya sheria hii ni kuendeleza shughuli za uvuvi na kudhibiti uvuvi haramu kama vile matumizi ya baruti, bunduki na nyavu za macho madogo. Sekta ya Uvuvi ina nafasi kubwa ya kuinua uchumi wa Zanzibar iwapo sekta hiyo itaendelezwa kikamilifu. Idara ya Uvuvi inao wajibu wa kuhakikisha kuwa sheria na kanuni za uvuvi zinasimamiwa ipasavyo ili wananchi waweze kunufaika na rasilimali za baharini. Tunashuhudia meli za uvuvi hasa za kigeni zinakuja kuvua samaki katika bahari ya Zanzibar bila ya kuwa na kibali kinachotakiwa. Hali hii inaikosesha serikali mapato ya sekta ya uvuvi. Serikali itajitahidi kuipatia Idara ya Uvuvi vitendea kazi ili iweze kusaidiana na vyombo vya ulinzi na usalama kufanya doria katika bahari kuu ili kukabiliana na wizi wa samaki katika bahari yetu.

Mhe. Spika, katika kuongeza mapato ya sekta ya uvuvi, Idara ya uvuvi inatakiwa kuangalia viwango vya kodi zinazotozwa kwa meli za kigeni zinazovua katika bahari ya Zanzibar. Kiwango cha kodi kinachotozwa sasa, kwa kweli ni kidogo sana ikilinganishwa na samaki waovuliwa pamoja na bei ya samaki katika soko la kimataifa.

Mhe. Spika, ili sekta ya uvuvi iendelee na iweze kutoa mchango mkubwa katika kukuza pato la Taifa, Waheshimiwa Wawakilishi wameishauri serikali ifanye mambo 4 yafuatayo.

1. Serikali ifanye juhudi za kuwavutia wawekezaji wa uvuvi wa bahari kuu.

2. Pili, serikali itafute wawekezaji wa viwanda vya kusindika samaki.
3. Serikali ianzishe maabara ya kukagua ubora wa samaki.

4. Serikali ianzishe Chuo cha Uvuvi ili kuwapatia vijana ujuzi katika masuala ya uvuvi.

Serikali imeupokea kwa moyo mkunjufu ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe na kuhakikisha kwamba utaufanyia kazi ipasavyo kwa lengo la kuimarisha sekta ya uvuvi na maendeleo ya Zanzibar kwa ujumla.

Halikadhalika, Baraza lako tukufu lilipata fursa ya kujadili Kura ya Maoni kuhusu kuanzishwa kwa mfumo wa Serikali Umoja wa Kitaifa. Sheria ya Kura ya Maoni itaipa mamlaka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kusimamia maandalizi ya Kura ya Maoni. Kufanyika kwa Kura ya Maoni ni matokeo ya maamuzi yaliyofanywa na Baraza lako tukufu kupitia Hoja Binafsi juu ya pendekezo la kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar katika Baraza lililopita.

Mhe. Spika, kama mnavyojua maridhiano ya kisiasa kati ya Rais Karume na Maalim Seif Sharif Hamadi yamefungua milango ya maelewano kati ya Chama cha Mapinduzi na CUF. Tunamshukuru sana Rais Karume kwa umahiri wake, kwa juhudi anazozichukua katika kuleta utengamano na amani hapa Zanzibar *(Makofi)*.

Amani na utulivu bila ya shaka vitatusaidia sana kuvutia wawekezaji mbali mbali kuja kuwekeza hapa Zanzibar. Zanzibar imebarikiwa sana na muumba kuwa na mandhari nzuri sana kwa shughuli za kibiashara. Tunayo fursa ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo muhimu cha biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki. Zanzibar inao uwezo wa kuwa Dubai ya Afrika ya Mashariki iwapo Wazanzibari watadhamiria kudumisha amani. Mipango na ndoto zetu za maendeleo hazitaweza kufikiwa bila ya kuwepo amani na utulivu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa mara nyingine tena Zanzibar inafungua ukurasa mpya katika historia ya medani ya demokrasia. Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa miongoni mwa nchi chache katika ukanda wa Afrika Mashariki kuanzisha utaratibu wa kuwa na Kura ya Maoni katika kutoa maamuzi ya masuala mazito ya kitaifa, kama sikoei miaka michache iliyopita wenzetu Kenya walifanya Kura ya Maoni.

Kufanyika kwa Kura ya Maoni kumevutia hisia kubwa sana za watu wengi ndani na nje ya Zanzibar. Wazo la kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa si geni hapa Zanzibar. Wazo hili liliwahi kuzungumzwa na Marehemu Mwalimu mwaka 1995 kwa mara ya kwanza. Suala hili lilizungumzwa tena katika Muafaka wa Kwanza wa mwaka 1999. Kwa bahati mbaya Muafaka ule

haukutekelezwa kama ilivyotarajiwa. Vile vile suala la kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa lilijadiliwa tena katika Muafaka wa Pili mwaka 2001.

Halikadhalika, wazo la kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa lilizungumzwa tena mwaka 2008, wakati wa mazungumzo baina ya Chama cha Mapinduzi na CUF huko Bagamoyo. Mapendekezo ya mazungumzo ya Bagamoyo yalipelekwa katika vikao vya Chama cha Mapinduzi na kujadiliwa katika Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa kilichokutana Butiama mwaka huo wa 2008. Kikao hiki kiliamua kuwa suala la kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni jambo la busara, lakini linapaswa kuamuliwa na wananchi kwa kupitia Kura ya Maoni.

Mhe. Spika, viongozi wa nchi yetu tokea wakati huo wamekuwa wakichukua hatua mbali mbali, ili kupata suluhu ya kudumu ya mgogoro wa kisiasa Zanzibar. Marafiki wa Zanzibar, wasomi, viongozi na wananchi wamekuwa wakisononeka sana wanapoona Wazanzibari wenyewe kwa wenyewe wanaumizana kila unapofanyika uchaguzi Mkuu. Viongozi walio makini hawawezi hata siku moja kuyapuuza mawazo yanayopendekeza kutafutwa njia bora ya kuleta maelewano na utengamano miongoni mwa wananchi.

Kwa kuwa Sera za CCM zinasisistiza juu ya amani na umoja miongoini mwa wananchi, viongozi wa chama hicho wanapaswa kuwa mstari wa mbele kutafuta amani na utulivu. Chama chetu kinafanya hivyo kwa sababu sisi ndio tuliopewa dhamana ya kuiongoza nchi yetu kwa sasa. Katika hali hiyo viongozi wetu watakuwa watu wa ajabu sana wakiiacha nchi iingie kwenye vurugu.

Vurugu hazina tija zinaleta maafa, vifo, uharibifu wa mali na ufukara katika nchi. Fujo siku zote hazina tija, kwa sababu wawekezaji waliomakini hata siku moja hawawezi kuwekeza kwenye nchi yenye matatizo ya kisiasa.

Uzoefu unaonesha kwamba viko vitu vitatu katika nchi ambavyo haviwezi kupatikana kwenye nchi yenye vurugu. Kwanza wanazuoni na wasomi, ukienda kwenye nchi na kukuta wanazuoni na wasomi wanaondoka, basi ujue hapo kuna vurugu. Ukienda pahala ukiona mitaji mikubwa matajiri wanakimbia ujue mahala hapo kuna vurugu.

Vile vile ukienda sehemu nyengine ukaona maendelea yanakuwa duni, basi ujue sehemu hiyo kuna matatizo. Sasa hapa tulipofika Zanzibar tumefikia mahala wasomi na wanazuoni wanagongana sasa kuja Zanzibar, mitaji inakuja Zanzibar na maendeleo *Alhamdulillah* tunamshukuru Rais Karume kwa kazi nzuri. Kwa hivyo, hii ni dalili kwamba njia tunayoelekea inayo mwanga wa matumaini *(Makofi)*.

Mhe. Spika, sisi viongozi sote wa serikali na vyama, tunao wajibu mkubwa sana kwa Mwenyezi Mungu muumba na wananchi waliotupa dhamana kuwatumikia na kutetea maslahi ya wananchi. Hata hivyo, pamoja na kuwatakia wananchi wetu mambo mema na yaliyomazurii hatuna uwezo hata siku moja wa kuwalazimisha.

Namfananisha kiongozi na mtu mwenye tochi anayewamurikia wenziwe walioko kwenye giza, anaweza kufanya hivyo kama wale watu wanatamani mwanga, lakini wakimwambia wanahitaji giza kwa shughuli zao, basi hawezi kuwalazimisha kuwapa mwanga na viongozi ndio hivyo hivyo.

Kazi ya viongozi ni kuwaeleza watu mambo yaliyomema, lakini wajibu wa kukubali ni kazi ya wananchi na wala hakuna mwenyekuweza kuwalazimisha kazi yetu. Isipokuwa ni kuwashawishi wananchi kwa maneno matamu, lakini wasipokubali hatuwezi kuwalazimisha hata siku moja *(Makofi)*.

Ndio maana lilipokuja wazo la kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika vikao vya CCM, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi walisema jambo hili ni zuri ila wapelekewe wananchi waamue. Iwapo wananchi watakubali wazo hili, basi serikali itaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 na Kinyume chake basi serikali haitafanya hivyo.

Mhe. Spika, najua wapo baadhi ya watu wanaozunguka na kuwaambia wananchi kuwa uamuzi wa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa tayari umeshafanywa. Jambo hili si Kweli. Bado uamuzi huo haujafanywa mpaka sasa. Mwezi Januari tulijadili hoja ya kufanya Kura ya Maoni kwa kupitia Hoja Binafsi.

Katika kikao hiki tumepitisha mswada wa sheria ya kuitaka Tume ya Uchaguzi kuandaa Kura ya Maoni, ili kuwauliza wananchi iwapo wanataka au hawataki iundwe Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ninarudia Serikali ya Chama cha Mapinduzi hakijafanya uamuzi wowote wa kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tunasubiri maoni ya wananchi ndio yatakayoamua ama tuanzishe au tusianzishe Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, Kura ya Maoni ni utaratibu unaotumiwa na nchi nyingi zenye demokrasia iliyoshamiri katika kutoa uamuzi muhimu ya kitaifa. Nchi hizi zinapendelea Kura ya Maoni kwa sababu ni demokrasi ya moja kwa moja, kuliko ile demokrasia ya uwakilishi kupitia Mabaraza ya Kutunga Sheria. Wapo baadhi ya wasomi wanaosema uamuzi wetu hauna maana na tunapoteza fedha za walipa kodi bure.

Sisi Wawakilishi tulipaswa tuamue kwa niaba ya wananchi. Ni kweli, lakini busara inaonyesha kwamba kuwashirikisha wananchi wote katika maamuzi

mazito ya jinsi wananchi hao wanavyotaka waongozwe ni jambo lililobora zaidi. Mbona wale waliotufundisha demokrasia wanafanya Kura za Maoni wakati nchi hizo zinapokuwa na masuala mazito ya kuamuliwa pamoja na kwamba Mabunge ya Kutunga Sheria yapo *(Makofi).*

Hata hivyo, nakubaliana na wale wanaosema Kura ya Maoni inahitaji kuandaliwa kwa umakini wa hali ya juu sana, ili kuleta matokeo yaliyotarajiwa. Hili ni jambo la msingi ninahakika Tume ya Uchaguzi italizingatia kwa makini sana. Vile vile wananchi wanapaswa waelimishwe kiasi cha kutosha, ili pale watakapotaka kufanya maamuzi basi wafanye maamuzi ya busara na hekima bila ya kuburuzwa na wale wanaopitapita. Hii ndiyo kazi inayoikabili Tume ya Uchaguzi, ninahakika tume hiyo itaifanya kazi hii kwa welezi wa hali ya juu sana *(Makofi).*

Mhe. Spika, chama chochote cha siasa kinayo Katiba pamoja na sera za msingi, ambazo zinawashawisha wananchi kujiunga na kuamini falsafa ya chama hicho. Sera za msingi za Chama cha Mapinduzi ni kutetea haki hasa za wanyonge, kupigania na kutetea amani, umoja na maendeleo ya taifa.

Wapo baadhi ya waumini wa vyama vya siasa, wanaziamini sera za vyama vyao kwa kauli, lakini ndani ya mioyo yao kidogo wanapata kigugumizi. Kwa hivyo, inatakiwa matamko ya mdomo ya kuamini sera na imani ndani ya moyo viende sambamba, ili utekelezaji uwe mzuri zaidi *(Makofi).*

Mhe. Spika, kuna kiongozi mmoja aliwahi kunipa hadith moja ya hatari ya kutamka jambo, lakini kutokuamini ndani ya moyo, kwa kweli alinipa hadith hiyo ya kusisimia sana ambayo inasema hivi. Yupo mwalimu mmoja wa madrasa na wanafunzi wake katika kila somo yule mwalimu anawaambia wanafunzi wake, wanafunzi msifanye mas-hara wakati wa kusoma *Quraan*, Mwenyezi Mungu ukimuamini kwa dhati ndani ya moyo, basi unaweza kutembea juu ya maji ya bahari.

Sasa akawepo mwanafunzi mmoja na ile kauli akawa anairudia na kumuuliza mwalimu kweli, alimwambia kweli muhimu tafuta maji yaliyosafi ujitie udhu na halafu uwe unapita baharini basi utakwenda tu, alimwambia mpaka kwenye kina kikubwa cha bahari utafika, alimwambia ndio bila ya shaka hakuna wasi wasi.

Kwa hivyo, yule mwanafunzi alisikiliza kwa makini sana. Sasa siku moja yule mwanafunzi alikuwa na boti, kwa bahati mbaya siku moja wakati anataka kwenda kuvua akaangalia mafuta kwenye boti na kuona yamemalizika, basi aliona atumie ile elimu ya mwalimu wake ya kuamini ndani ya moyo.

Sasa mwanafunzi yule alikwenda katika maeneo ya jirani na kutafuta maji safi na kutia udhu, baada ya kuweka udhu basi kweli alikwenda na kufika baharini kwenye kina cha maji na kuvua samaki na siku hiyo Mwenyezi Mungu alimbariki alipata samaki wengi sana.

Baada ya kurejea wale samaki nusu alimpelekea mwalimu wake kutokana na furaha yake, basi aliendelea kufanya hivyo kwa muda wa mwezi mzima ah! Yule mwalimu akaanza kupata wasi wasi na kusema kuna mtu hapa anataka kuniharibia nyumba mbona samaki wanaletwa kila siku alimuuliza mkewe nani huyu, mkewe alimwambia kuna yule kijana wako ambaye ni mwanafunzi wako anaitwa Juma.

Kutokana na hali hiyo, jioni yake alimtafuta Juma, lakini sio Maalim Juma Duni ni Juma mwengine. Ah! Alimuuliza yule mwanafunzi wake umefanya nini mbona neema zimeongezeka, alimwambia mwalimu elimu yako hii, elimu yangu vipi na mimi sivui. Kwa hiyo, alimwambia siku moja ulitwambia sisi kama mtu anamuamini Mwenyezi Mungu kwa dhati basi anaweza kutembea juu ya maji ya bahari na wala hatozama.

Kwa hivyo, mimi nimemuamini na nimetia udhu, basi sasa kwa muda wa mwezi mzima nafanya biashara hii na nafanikiwa hivi, yule mwalimu alimwambia wacha mas-hara yako. Ah! Huyu ndiye aliyeniambia kwamba nikimuamini Mwenyezi Mungu nitatembea juu ya maji, alimwambia wacha mas-hara yako, alimwambia sifanyi mas-hara nakuzungumza kwa dhati basi tufutane.

Sasa siku moja wakafuatana, yule mwanafunzi alijitia udhu na baadaye alimwambia yule mwalimu wake ajitie udhu, safari kuanza kiasi mita kama ishirini mwalimu akaanza kuzama, basi yule mwanafunzi alirudi na kumuokoa mwalimu wake.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba inaonekana mwalimu alitamka, lakini pengine hakuamini.

Mhe. Spika, serikali zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi thabiti wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Rais Amani Karume, zilianzisha mfumo wa kuwawezesha wananchi unaojulikana kwa jina maarufu la mfuko wa JK na AK, ili kuwawezesha wajasiriamali kukuza biashara zao.

Katika mkutano uliopita niliwaahidi Waheshimiwa Wajumbe kutoa taarifa ya maendeleo ya utoaji mikopo ya uwezeshaji wa wananchi. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa mpaka mwezi wa Februari jumla ya shilingi milioni 827 zimekopeshwa kwa wajasiriamali 408 katika mikoa mitatu ya Unguja.

Napenda kutoa mchanganuo kama ufuatavyo:-

1. Wilaya ya Kaskazini ‘A’ zimetolewa shilingi milioni 74,
2. Wilaya ya Kaskazini ‘B’ zimetolewa shilingi milioni 139,
3. Wilaya ya Kati zimetolewa shilingi milioni 56,
4. Wilaya ya Kusini zimetolewa shilingi milioni 54,
5. Wilaya ya Magharibi zimetolewa shilingi milioni 373 na
6. Wilaya ya Mjini zimetolewa shilingi milioni 128.

Kwa ujumla ni ndizo hizo shilingi milioni 827.

Kwa upande wa Mikoa miwili ya Pemba jumla ni shilingi milioni 336 zilitolewa kwa vikundi 545 kwa mgawayo ufuatao:-

1. Wilaya ya Wete zilitolewa shilingi milioni 81,
2. Wilaya ya Micheweni zilitolewa shilingi milioni 44,
3. Wilaya ya Mkoani zilitolewa shilingi milioni 49 na
4. Wilaya ya Chakechake zilitolewa shilingi milioni 162.

Kwa ujumla ndizo hizo shilingi milioni 336.

Mhe. Spika, utoaji wa mikopo unafanywa kwa kufuata masharti yaliyowekwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Ulipaji wa madeni tayari umeshaanza. Nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wanaolipa mikopo, ili kuwawezesha wananchi wengine nao kufaidika na mikopo hii.

Naziomba taasisi zote zinazohusika na mikopo ya Rais Jakaya Kikwete na Rais Amani Karume kuhakikisha wanafanya kazi na wanaimarisha utendaji wao wa kazi, ili uwe wa ufanisi zaidi. Usimamizi mzuri utasaidia kudhibiti vitendo vya udanganyifu katika utoaji wa mikopo. Natambua kuwa bado yapo majimbo ambayo watu wake hawajapata mikopo hiyo.

Mhe. Spika, ninawaahidi Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo hayo kuwa nitahakikisha majimbo hayo nayo yanaangaliwa kwa jicho la huruma, ili kuleta usawa. Nitaendelea kukutana Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Maafisa wa Benki ya Watu wa Zanzibar na Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, ili tujadili matatizo yanayojitokeza katika utoaji mikopo. Mwezi huu nitaonana na viongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Hivi sasa tayari nimeshaonana na viongozi wa Mikoa miwili ya Pemba pamoja na Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, wapo Waheshimiwa Wajumbe ambao walitamani sana kupewa orodha ya miradi ambayo imeshapatiwa fedha hizi za mikopo ya JK na AK.

Kwa bahati mbaya orodha ile ni ndefu sana na ingenichukua muda mrefu sana kuisoma hapa.

Lakini nitakapokutana na viongozi kwenye ngazi hiyo ya wilaya na mikoa nitajitahidi sana kutoa nakala kwa ajili ya hao viongozi, kila tunapokutana sasa tuzitizame ili tujue hasa majimbo yepi tayari yameshapata mikopo hiyo na yepi bado. Kwa hivyo, maafisa wa benki watupe sababu majimbo hayo kwa nini hayajapata mikopo hiyo watueleze. Nadhani bila ya shaka vikao vya namna hii vinasaidia sana katika kurahisisha utendaji.

Mhe. Spika, nakumbuka kulikuwa na wakati Mhe. Ame Mati Wadi alikuwa akilalamika sana hapa, sasa tulipofanya mkutano ule na viongozi wenzake wa mkoa tulipata njia kidogo sisemi kama mambo yamekuwa mazuri sana, lakini kuna mwanga wa matumaini kidogo na hali si mbaya sana *(Makofi)*.

Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba, tutajitahidi kufanya kila lililokwenye uwezo wetu, kwa ajili ya kuhakikisha kuwa utoaji wa mikopo hii unakwenda vizuri kama ilivyopangwa *(Makofi)*.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa natamka rasmi kuwa Baraza lako Tukufu liakhirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 09 Juni, 2010 saa 3.00 asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Waziri Kiongozi kwa hotuba hiyo uliyoitoa na wajumbe tumeisikia na tunakupongeza kwa nasaha zako *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri Kiongozi wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kumshukuru Mhe. Waziri Kiongozi, sasa niakhirishe Mkutano huu wa Kumi na Tisa hadi siku ya Jumatano 9 Juni, 2010 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 7:25 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 09/06/2010 saa 3:00 asubuhi)